

HABARI ZA MANABII


(MWALIMU)



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Pili



HABARI ZA MANABII

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

(MWALIMU)

Mwaka wa Tatu

Kitabu cha Pili

Africa Coordinated Curriculum for
Bible Study

J3 - 2Ts

Used by permission of International Publications Services

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, NAIROBI

© Copyright, 1987
Baptist Publications House
All rights reserved

YALIYOMO

SURA

UKURASA

1. Je! Manabii ni Nani?	5
2. Eliya, Nabii Mwenye Ujasiri	10
3. Amosi Ahubiri Juu ya Hukumu ya Mungu	16
4. Hosea Anaeleza Upendo wa Mungu	21
5. Isaya Aliitwa Kutoa Habari Njema	25
6. Mika Anaeleza Mahitaji ya Mungu	29
7. Neno la Bwana Lamjia Sefania	33
8. Nahumu Nabii wa Maangamizi	38
9. Habakuki, Nabii wa Maswali	44
10. Mpango wa Mungu kwa Yermia	49
11. Swali la Malaki: "Je! Mwanadamu Atamwibia Mungu?"	54
12. Mungu Anawapenda Watu Wote	58
13. Kuwa na Ujasiri Wakati wa Hatari	63

UJUMBE KWA MWALIMU

Baadhi ya watu wanafikiria kwamba wanaweza kufurahia kusoma Agano Jipya kuliko Agano la Kale. Lakini wale waliosoma sana Agano la Kale wanajua kwamba ni sehemu muhimu sana ya Biblia. Kwa kweli, mtu hawezi kuelewa kamwe Agano Jipya hadi aelewapo kwa ukamilifu Agano la Kale.

Wakati mtu asomapo Agano la Kale hujifunza jinsi Mungu alivyowaita watu wa taifa la Israeli. Kuna hadithi za kupendeza zihusuzo watu wenye ujasiri mkuu. Humu ndimo tupatapo ukweli uhusuo waliowaovu.

Ujumbe wa manabii waliotumwa na Mungu unapatikana katika Agano la Kale. Manabii hawa waliitwa na Mungu ili wawaonye watu juu ya dhambi zao. Walizungumzia jinsi watu hao wangeangamizwa iwapo hawangeacha kutenda maovu. Walileta pia ujumbe wa tumaini. Walizungumzia pia juu ya upendo wa Mungu. Walisema kwamba angemtuma mfalme mkuu kuliko Daudi. Naye ange-mwezesha mwanadamu kupata wokovu.

Wewe kama mwalimu wa vijana wakubwa utakuwa na nafasi ya kuwasaidia wanafunzi wako waone kama kwamba manabii hawa “wangali hai”. Kiini cha masomo haya ya miezi mitatu ifuatayo ni, “Mafunzo juu ya Manabii.” Somo la kwanza litaeleza kwamba manabii walikuwa watu wa aina gani na sababu zilizomfanya Mungu awaite (awachague). Hatuna muda wa kutosha wa kujifunza juu ya manabii wote, lakini utawaongoza wanafunzi wako katika kujifunza habari za manabii wote, lakini utawaongoza wanafunzi wako katika kujifunza habari za manabii kumi na wawili. Kila somo litasimulia juu ya maisha na ujumbe wa nabii mmoja. Utapaswa kuwasaidia wanafunzi wako waweze kuelewa sababu iliyowafanya wasome ujumbe huo. Utapaswa pia kuwasaidia kuona kwamba ujumbe huu wa manabii ungali wa muhimu hata kwetu.

Somo hili la Agano la Kale laweza kuwa la kuvutia na lenye manufaa!

SURA YA KWANZA

JE! MANABII NI NANI?

MASOMO YA BIBLIA: Jeremiah 1:4-8; 2 Petro 1:20-21

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wako: Je! wanajua nini kuhusu manabii? Je, wanafikiria kwamba nabii ni kama mtabiri?

Somo hili litakupa fursa ya kuweza kuwaongoza wanafunzi wako kuwaza kuelewa aina ya watu ambao walikuwa manabii wa Agano la Kale.

Watoto huwa wanaweza kukumbuka hadithi ya Biblia, lakini hasa huwa hawajui wakati ilipotokea. Hawajui wakati wafalme au manabii waliishi. Kwa hivyo usitarajie kwamba watoto hawa wataweza kukumbuka miaka hiyo. Hata hivyo, wanapaswa kujifunza jinsi mambo ya Biblia yalivyokuwa ya kifuatana. Somo hili litaweza kuwasaidia kuelewa wakati na kwa nini Mungu aliwaita manabii wa kumtumikia.

Soma Maandiko ya Biblia. Soma kila kitu kilichoko katika somo hili na katika somo la kitabu cha wanafunzi.

Utapaswa kusoma kitabu cha 1 Samweli, hasa Sura ya 8 ili ujue sababu zilizomfanya Mungu kuwaita manabii. Samweli alimtumikia Mungu kwa njia mbali mbali. Alikuwa kuhani ambaye alimtotea Mungu dhabihu. Alitumikia pia kama hakimumu aliyetoa uamuzi uhusio sheria. Alikuwa pia nabii, yaani alinena kwa niaba ya Mungu.

Watu walimjia Samweli na kumwambia kwamba wanataka Mfalme ambaye atawaongoza. Walitaka wawe kama mataifa jirani.

Mfalme wa kwanza alikuwa Sauli. Kulingana na desturi za wakati wa Sauli, mtu alipewa ufalme kwa sababu baba yake alikuwa mfalme. Walikuwa wakiurithi ufalme kutoka kwa baba yao. Baadhi ya watu hawa walikuwa waovu sana. Mungu alimhitaji mtu ambaye angewaambia watu ujumbe wake. Kwa hivyo, alimwita nabii ili anene kwa niaba yake. Baadhi ya Wafalme walifikiria tu juu ya utawala na utajiri. Lakini manabii hawakuwa kama wafalme. Wao walimwamini Mungu naye Mungu angewategemea wao kwa kuwaambia watu ujumbe wake.

Vifungu vya kwanza vya Biblia, yaani, Jeremiah 1:4-8, vinatambua jinsi Mungu alivyomwita nabii mmoja. Nabii wa kweli ni yule aliyesema ujumbe wa Mungu. Mungu ndiye aliyemwita na kumpa ujumbe huo.

Watu wengi wanafikiria kwamba nabii ni yule mtu ambaye ataweza kutabiri kile kitakachofanyika baadaye. Manabii wa Kiebrania hawakujishughulisha hasa na kazi hii. Walikuwa wakiwaeleza watu juu ya mapenzi ya Mungu waliposema nao. Hawakusema yale wanayofikiria wenyewe. Walisema ujumbe wa Mungu ambaye ndiye aliyewaita.

Kulikuwa na watu wengine walioitwa “manabii wa uongo”. Wao walisema yale ambayo yaliwapendeza watu. Lakini wale manabii ambao ujumbe wao uko katika Agano la Kale ni watu ambao walikuwa wanamjua Mungu. Waliishi maisha yao kwa kumtegemea Mungu Walimtarajia kusema nao. Mungu aliwaita manabii hawa. Alisema nao na akawapa ujumbe wa kuwahubiria watu.

Petro wa Pili 1:20-21 inatuambia kwamba manabii hawakusema yale waliyofikiria wenyewe. Roho Mtakatifu aliwapa ujumbe wa Mungu. Kusudi lao la kuhubiri lilikuwa ni kuwasaidia watu kumjua Mungu aishiye.

Ujumbe wa manabii 17 unapatikana katika Agano la Kale. Hebu tazama orodha iliyoko katika kitabu cha wanafunzi. Hakuna ajuaye miaka kamili ambayo watu hawa waliishi na kuhubiri. Hata hivyo, orodha hii itakusaidia kuelewa kwamba manabii hawa walinena ujumbe wao wakati kuwepo kwa wafalme. Wengine nao walihubiri baada ya Israeli na Yuda kutekwa na maadui zao.

Watu kama Nathani, Eliya na Elisha walikuwa pia manabii. Waweza kusoma habari zao katika 2 Samweli na Wafalme wa Kwanza na wa Pili.

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwamba manabii wa Agano la Kale walikuwa watu wa aina gani na sababu zilizomfanya Mungu awaite.*

KULIFUNDISHA SOMO

Waambie wanafunzi wakisikilize. Andika ubaoni au kwenye karatasi kubwa swali hili: Je! manabii ni nani? Wape muda wa kusema yale wanayofikiria juu ya swali hili.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome aya ya kwanza katika kitabu chake iliyo na kichwa hiki: “Je! Nabii ni Nani?”

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yeremia 1:4-8. Sasa eleza kwa nini Mungu aliwaita manabii.

Sema: “Watu wa Israeli walitaka kuwa na wafalme wa kuwaongoza. Lakini wafalme wengi walikuwa wanataka tu utajiri na mamlaka ya taifa lao. Watu walianza kuabudu miungu na sanamu. Mungu Yehova alimhitaji mtu wa kuwaonyesha watu hawa dhambi zao. Alimhitaji mtu kuwakumbusha juu ya agano lao walilofanya na Mungu. Israeli ilikuwa imekubali kumwabudu Mungu Yehova na kufuata amri zake.

Uliza: Je! Inamaanisha nini tunaposema kwamba nabii ni “Mtabiri?” (Ni yule ambaye anazungumzia yale ambayo Mungu anawafikiria watu wake na matendo yao.)

Sema: Ni kweli kwamba manabii walisema yale ambayo yangetokea iwapo hawakutii neno lake. Hivyo basi, manabii nao wanaweza kuitwa “watabiri”.

Waruhusu wanafunzi waandike vitabuni mwao maana ya nabii iwapo

hawajaandika. Waambie baadhi ya wanafunzi wasome majibu yao wamalizapo kuandika.

Mwambie mmoja wao asome 2 Petro 1:20-21. Jadilianeni swali hili. Je! nabii hupataje neno la Mungu?" (Tumia maelezo yaliyoko katika kitabu cha wanafunzi ambayo yanafuatia swali hili.)

Uliza: Je! "manabii wa uongo" walikuwa akina nani? Eleza kwamba baadhi ya dini zilikuwa na watu ambao walijaribu kuwashauri watu wao na kuwaambia kile ambacho kingetokea baadaye. Walitumia uganga. Hawakumjua Mungu wa kweli kwa hivyo hawangeweza kusema ujumbe wake. Kulikuwa pia na manabii wa uongo katika Israeli ambao walisema maneno yaliyopendeza watu. Kusudi lao kuu lilikuwa ni kupata pesa na kuwapendeza watu. Manabii wa kweli wa Israeli hawakukubaliana nao.

Uliza: Je! Manabii wa kweli walihubiri kuhusu nini? Wahimiza wanafunzi kutafuta jibu la swali hili katika vitabu vyao iwapo watashindwa kulijibu.

Sasa jadilianeni wakati ambao manabii hawa waliishi. Usiji-shughulishe sana na kusema miaka kamili. Lakini utapaswa kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa wakati ambapo manabii hawa waliishi na kutoa ujumbe wakati wa historia ya Israeli. Utapaswa kutumia orodha ifuatayo. Pengine utataka kukaza juu ya miaka ya historia ya Israeli iwapo unawafundisha vijana wakubwa.

Pengine itasaidia iwapo utanakili orodha hii ya mpango kwenye karatasi

kubwa. Ibandike kwenye ukuta darasani mwako na uwe unaitumia wakati unapofundisha.

Miaka ya Biblia	Viongozi na Wafalme	Manabii
1800 B.C.	Ibrahimu. (miaka na tarehe kamili haijulikani) Isaka	
1300-1200 B.C.	Musa, Haruni, Miriamu, Yoshua, Kalebu	
1020-922 B.C.	(Ufalme wa pamoja) Sauli, Daudi, Sulemani	Nathani, Eliya, Elisha
922-722 B.C.	(Ufalme uliogawanyika) Kulikuwa na Wafalme tofauti katika Yuda na Israeli	Yona, Amosi, Isaya, Mika, Hosea
722-587 B.C.	(Israeli ilishindwa mnamo mwaka wa 721 B.C.) Wafalme wa Yuda	Zefania, Nahumu, Habakuki, Yeremia
587-400 B.C.	(Yuda ilishindwa mnamo mwaka wa 587 B.C.) Zerebabeli, Nehemia, Ezra	Danieli, Ezekieli, Hagai, Zekaria, Obadia, Malaki
400-6 B.C.	Makabusi, Mfalme Herode	Yoeli
6-4 B.C.	Mfalme Herode	

KAZI YA KUFANYA

Rudia na mjibu pamoja maswali haya yaliyo na yasiyo ya kweli.

Andika herufi ya K kando ya sentensi zote zilizo za kweli na herufi ya L kando ya sentensi zisizo za kweli.

1. K Nabii wa kweli alikuwa yule aliyesema ujumbe wa Mungu.
2. L Manabii wengi wa Kiebrania waliishi baada ya kuzaliwa kwa Yesu.
3. L Mungu aliwachagua wafalme wote wa Israeli na Yuda.
4. K Kulikuwa na manabii wa uongo wa Kiebrania waliyosema yale ambayo watu walipenda kuyasikiliza.
5. K Manabii wa kweli wa Kiebrania waliwahubiria watu juu ya hukumu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zao.

Rudia sehemu mbali mbali za vitabu vya Biblia jinsi vilivyoonyeshwa pichani. Waambie wanafunzi wako kuanza kukariri majina ya vitabu vya manabii. Pengine utapanga kufanya mashindano katika miezi hii mitatu ili uwahimiza wanafunzi wako kuweza kukariri.

Eleza maana ya nabii mdogo na nabii mkubwa. (Wale manabii kumi na mawili wanaitwa manabii wadogo kwa sababu waliandika ujumbe mfupi. Hawaitwi manabii wadogo kwa sababu ujumbe wao si muhimu kama ule wa manabii walioandika maneno mengi. Manabii wale wengine wanaitwa

manabii wakubwa kwa sababu waliandika ujumbe mwingi.)

Tazama picha ifuatayo ya rafu ya vitabu. Utaweza kuona majina yote ya vitabu vya Biblia. Je! ni vitabu vingapi? 66

Orodha iliyoko katikati ni ya vitabu vya manabii. Vitabu vitano vilivyoko upande wa kushoto ni vya manabii wakubwa, na vile kumi na viwili vilivyoko upande wa kulia, ni vya manabii wadogo.

Kulikuwa na watu wengine katika Agano la Kale ambao waliitwa "manabii wa zamani." Hakuna vitabu kamili ambavyo vina majina yao. Lakini tunaweza kusoma habari zao katika vitabu vya historia. Tutajifunza juu ya mojawapo wa watu hawa aitwaye Eliya, katika somo lifuatalo.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mungu ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii..."
(Waebrania 1:1).

Waongoze wanafunzi katika kujifunza kusema kifungu cha kukumbuka. Pengine utataka kuweka rekodi za wale ambao wanaweza kukariri kifungu cha kukumbuka cha kila somo.

Waambie wanafunzi wako kwamba wataweza kujifunza jinsi Mungu alivyonena kupitia kwa manabii na yale aliyosema kwa muda wa wiki kumi na mbili zifuatazo. Ujumbe huu ulisemwa kwa watu miaka mingi iliyopita, lakini ungali wa muhimu hata kwetu. Maovu mengi yaliyokuwepo siku hizo yangalipo pia siku hizi.

WAKATI WA MWISHO

Hebu tazama tena kusudi la somo hili. Je! unadhani kwamba wanafunzi hao wanaelewa aina ya watu ambao walikuwa manabii wa Agano la Kale na sababu zilizomfanya Mungu awaite?

Waambie waulize maswali yo yote ambayo wanayo. Pengine utatakiwa kutumia muda mfupi kwa kurudia majibu ya maswali yafuatayo:

1. Je! nabii ni nani?
2. Je! nabii hupataje neno la Mungu?
3. Je! manabii walihubiri juu ya nini?
4. Je! manabii waliishi wakati gani?

Funga mkutano kwa maombi ya kumwomba Roho Mtakatifu akuongeze wewe pamoja na wanafunzi kuweza kujua manabii wa Agano la Kale kama watu wa kweli. Omba kwamba ujumbe wao utakuwa wa muhimu maishani mwetu.

ELIYA, NABII MWENYE UJASIRI

MASOMO YA BIBLIA: 1 Wafalme 17:1; 18:1-2, 20-24, 36-39

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wanafunzi wako wamekuwa wakihudhuria darasa kila wakati? Iwapo hawakuwa wakihudhuria, je! unajua ni kwa nini? Pengine wamekuwa wagonjwa au wamepatwa na matatizo mengine. Panga wakati mzuri wiki hii ambao utaweza kuwatembelea wale waliokosa kuhudhuria. Wajibu wako kama mwalimu ni zaidi ya kuwafundisha tu. Unapaswa kujua mahitaji ya wanafunzi wako. Unapaswa pia kujuana na watu wa jamaa yake. Sasa, ombea kwanza washiriki wa darasa lako ambao unajua wana matatizo fulani kabla ya kuendelea na somo hili.

Je! wanafunzi wako wanavutiwa na masomo hayo yahasuyo manabii? Jibu la swali hili ni juu yako wewe mwenyewe kama mwalimu. Tumia madokezo yaliyotolewa katika sehemu ya "kulifundisha somo". Waweza kuongezea mawazo yako mwenyewe. Usiongee tu kila wakati, lakini watie moyo wanafunzi wako waweze kujibu na kuuliza maswali. Jifunze hali ya maisha ya kila nabii hadi utakapojisikia kwamba umemjua kabisa nabii huyo. Utafanya somo hili liwapendeze wanafunzi, ikiwa wewe mwenyewe unalifurahia.

Ulipewa orodha ionyeshayo wakati kila nabii alipoishi katika somo la wiki iliyopita. Je! ulinakili au kuandika

orodha hii kwenye karatasi kubwa? Ikiwa hujaiandika, hakikisha kwamba umetumia orodha iliyoko kwenye kitabu chako kwa kuelezea wakati ambapo manabii hawa waliishi. Tumia pia ramani uliyopewa katika somo hili kuonyesha mahali ambapo falme hizi mbili zipo -- Israeli na Yuda.

Itumie kwa kuelezea mahali ambapo manabii hawa waliishi na watu ambao waliwahubiria. Hadithi ya Eliya inaweza kupatikana katika 1 Wafalme 17 hadi 2 Wafalme 2. Utafaidika sana iwapo utasoma sura hizi zote. Somo la leo linahusu yale yaliyofanyika katika sura ya 18.

Kuna mambo machache katika Biblia ambayo ni ya kutia ajabu sana kuliko kule kushindana kwa Eliya na manabii wa Baali kwenye Mlima Karmeli. Mungu alitumia Eliya kwa njia isiyo ya kawaida.

Biblia haituambii cho chote kuhusu Eliya kabla ya kufikia 1 Wafalme 17. Hapa ndipo anajulishwa kwa ghafula, kwa wasomaji wake. Miaka hamsini ilikuwa imepita tangu utawala wa Sulemani na kugawanyika kwa Israeli katika falme mbili. Ahabu alikuwa Mfalme wa saba ambaye alitawala sehemu ya kaskazini iliyoitwa Israeli. Naye Yehoshafati alikuwa mfalme wa ufalme wa kusini, yaani Yuda, wakati huu wa Ahabu.

Eliya alikuwa kama "dhamira" wa nchi yake. Aliongea juu ya uovu hata katika serikali. Alikuwa mtu mwenye

ujasiri. Alikuwa na ujasiri wa kuweza kuzungumzia matokeo ya dhambi na kumwachia Mungu kutoa matokeo ya mwisho. Kusudi lake kuu lilikuwa la kuwasaidia watu wa Israeli kuelewa kwamba Yehova ndiye aliyekuwa Mungu wa pekee.

Kuna aina mbili ya manabii katika Agano la Kale. Wa kwanza anakumbukwa kulingana na yale aliyofanya na wa pili anakumbukwa kutokana na yale aliyohubiri na kuandika. Biblia haina maandiko yote yalioandikwa na Eliya. Hata hivyo, wenzake wameandika kuhusu yale aliyofanya.

Ni habari chache sana inayojulikana juu ya Eliya kabla ya kwenda nyumbani kwa mfalme Ahabu na kumwambia juu ya ukame ambao ungetokea nchini kote (1 Wafalme 17:1). Kifungu hiki kinatambua kwamba Eliya alitoka mahali paitwapo Tishbi huko Gileadi. Kifungu kimoja kinatuelezea umbo la Eliya. Soma 2 Wafalme 1:8.

Maana ya jina la Eliya inalingana na ujumbe wake. Neno "Eliya" katika lugha ya Kiebrania linamaanisha "Yehova ni Mungu."

Kulikuwa hakuna dini ya kweli wala kuishi kwa haki katika taifa la Israeli. Mfalme Ahabu na mke wake mwovu, Yezebeli, walikuwa wameongoza taifa lao katika utendaji dhambi kuu. Walijenga sanamu za Baali kila mahali mle nchini. Ibaada za Baali zilikuwa ni pamoja na utoaji wa dhabihu (sadaka) ya kutekezeka ya mwanadamu hasa watoto. Wale watu ambao walimtii na kuwa waaminifu kwa Mungu Yehova, waliadhibiwa. Kwa hivyo, Mungu

alimtuma Eliya kutoa hukumu kwa watu wa Israeli.

Eliya alienda mbele ya Mfalme Ahabu na akamwambia kwamba hakutanyesha mvua kwa muda mrefu. Eliya alisema haya kabla ya wakati wa mvua kufika, kwa hivyo Ahabu hakuhangaishwa sana hadi mvua ilipokosa kunyesha.

Eliya alieleza kwamba ukame huo na njaa hii vingekuwa aina ya hukumu kwa taifa la Israeli. Mungu alikuwa akihukumu Israeli kwa kuabudu sanamu na miungu wa uongo.

Mungu alimtuma Eliya wakati huu wa ukame kwa kumpatia chakula na maji. Eliya alirudi Israeli baada ya miaka mitatu. Alimwambia wazi Ahabu sababu iliyomfanya Mungu kuleta kiu na njaa nchini kote. Shida ilikuwa kwamba watu wa Israeli walikuwa wamechanganya uabuduji wa Mungu na ule wa Baali.

Baadhi ya watu walianini kwamba Baali ndiye aliyetawala hali ya hewa. Watu walimwabudu kwa matumaini makubwa wakati wa njaa. Eliya aliona kwamba ni lazima watu wakate shauri kwamba watamwabudu nani – Mungu Yehova au sanamu za Baali.

Eliya alimwambia Ahabu kwamba watakuwa na mashindano kwenye Mlima Karmeli ya kuthibitisha ni yupi aliyekuwa Mungu wa kweli. Mashindano haya yangukuwa kati ya Eliya na manabii 450 wa Baali. Kila upande ungetoa sadaka ya kuteketewa. Jibu ambalo lingekuwa ni la kushuka kwa moto wa kuteketeza sadaka hiyo lingemthibisha Baali au Yehova kuwa ndiye Mungu wa kweli.

Manabii wa Baali ndio waliokuwa wa kwanza kutoa sadaka ya ng'ombe wao. Waliomba siku nzima ili mungu wao aiteketeze sadaka yao, lakini hawakufanikiwa. Ilipofika wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya alimwomba Mungu awadhihirishie watu kwamba yeye ndiye Mungu wa kweli. Bwana alimjibu. Moto wa Bwana ukashuka kutoka mbinguni na ukaiteketeza sadaka hiyo ya Eliya. Uthibitisho huu wa Mungu wa kweli uliwafanya watu waseme kwamba, "Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu." (1 Wafalme 18:39)

Eliya alikuwa na ujasiri mkuu kukabiliana na maovu, na kusema ujumbe ambao alipewa na Mungu. Wakristo wa siku hizi wanapaswa kuwa na ujasiri kama huu ili kukabiliana na maovu yaliyopo. Ujumbe wa Mungu u wazi siku hizi jinsi ilivyokuwa wakati wa Eliya.

Kusudi la somo hili *litawaongoza wanafunzi kuelewa kwamba wanapaswa kuwa na ujasiri wa kushinda maovu jinsi Eliya alivyoshinda.*

KULIFUNDISHA SOMO

Wagawe wanafunzi wako katika makundi mawili. Waambie kwamba watakuwa na mashindano ya kuonyesha ni kikundi kipi ambacho kinakumbuka vizuri majina ya vitabu vya manabii wakubwa na wale wadogo. Mpe mwanafunzi mmoja wa kila kikundi kalamu na karatasi. Mwambie mwanafunzi huyo aandike vitabu hivyo vya manabii wakati kikundi chake kinapovitaja. Makundi haya mawili yanatakiwa yawe mbali ili wasiweze

kusikia yale wenzao wasemayo. Wape dakika tano za kufanyia kazi hii. Liambie lile kundi lililo na majina mengi kusoma orodha yake.

Sasa tumia dakika chache kurudia na kujadiliana majibu ya maswali yafuatayo.

1. Je! nabii hufanya kazi gani?
2. Je! nabii hupata wapi ujumbe wake?
3. Je! nabii huhubiri kuhusu nini?
4. Je! manabii waliishi sana wakati gani?

Tumia orodha kubwa uliyotayarisha kwa kuonyesha miaka na wakati ambapo kila nabii aliishi. Ikiwa hukuweza kutayarisha orodha hiyo kwenye karatasi kubwa, waambie wanafunzi waiangalie orodha iliyoko katika somo la kwanza.

Sema: Hatujui miaka kamili ambayo kila nabii aliishi. Lakini, twajua kwamba Mungu alianza kuwatumia manabii kusema ujumbe wake baada ya kifo cha Mfalme Sulemani. Aliendelea kuwaita manabii hadi ilipobakia miaka michache kabla ya kuzaliwa kwa Yesu.

Waonyeshe jina la Eliya kwenye orodha hiyo.

Sema: Hamkuandika jina la Eliya mlipokuwa mkiandika majina ya manabii waliodumu na wale walikuwepo kwa muda mfupi. Hii ni kwa sababu Eliya hakuandika kitabu cho chote. Hata hivyo, unaposoma somo lako unaona kwamba mambo mengi yameandikwa juu ya Eliya katika 1 Wafalme 17 hadi 2 Wafalme 2.

Waambie wanafunzi wako waiangalie ramani iliyoko katika somo lao na watafute taifa la Israeli.

Sema: Israeli ilijulikana kama ufalme wa kaskazini. Huku ndiko Eliya aliishi na kuhubiri.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome ile sehemu ambayo Eliya anajitambulisha kwetu.

Uliza: Je! ni nini kilichokuwa kikifanyika Israeli ambacho kilimfanya Mungu amtume Eliya kwenda kwa Mfalme Ahabu? (Hakikisha umekaza kwamba watu walikuwa wakiabudu sanamu za Baali.)

Eleza jinsi Eliya alimwendea Mfalme Ahabu na kumwambia kwamba kutakuwa na ukame nchini.

Uliza: Je! mnafikiri jambo hili lilihitaji ujasiri?

Uliza: Je! Mfalme Ahabu na Malkia Yezebeli walikuwa watu wa aina gani? (Walikuwa waovu na wakatili.)

Uliza: Je! kunaye mmoja kati yenu ambaye anajua mahali ambapo Eliya aliishi wakati huu wa kukosa mvua?

Tumia dakika chache kwa kuelezea jinsi Mungu alivyomtunza Eliya karibu na kijito cha Korithi na jinsi alivyoishi nyumbani kwa mjane mmoja kule Sarepta. (1 Wafalme 17:2-24.)

Waonyeshe Mlima wa Karmeli kwenye ramani. Uko katika pwani ya Israeli juu ya herufi "L" katika "ISRAELI".

Uliza: Je! kunaye awezaye kusema kile kilichofanyika juu ya Mlima Karmeli?

Wape wanafunzi nafasi ya kusimulia mashindano yaliyodokezwa na Eliya. Utapaswa kusimulia jambo hili iwapo watahindwa kusema. Isiwasomee tukio hili, bali wasimulie kwa njia ya kuvutia. (Tazama 1 Wafalme 18:20-29 na sehemu iliyoko katika somo la wanafunzi chini ya kichwa hiki, "Ni Lazima Watu Waamue cha Kufanya.")

Unaweza kuwaruhusu wanafunzi waige mchezo wa yale yaliyofanyika kwenye Mlima Karmeli ikiwa kuna muda wa kutosha.

Kaza mambo yafuatayo unapondelea kufundisha sehemu hii.

1. Uabuduji wa miungu wa uongo ulikuwa ukiangamiza taifa la Israeli.
2. Mungu alimwita Eliya kumwonyesha kile kilichokuwa kikifanyika. Jambo hili lilihitaji ujasiri mkubwa.
3. Eliya aliwaita watu ili wakate shauri ni Mungu yupi ambaye watamwabudu.

Mtu hawezi kumfuata Mungu Yehova na awe mwaminifu kwa miungu ya sanamu. Mungu anahitaji utii na heshima zetu zote.

KAZI YA KUFANYA

Wasaidie wanafunzi katika kukamilisha fumbo hili la maneno. Majibu yake yamechorwa mviringo katika kitabu chako.

Je! unapenda kucheza mchezo? Kuna aina mpya ya mchezo hapo chini. Utapaswa kuwasaidia wanafunzi wako kupata majibu yaliyo sahihi.

Soma kila maandiko uliyopewa. Tafuta jibu la swali hilo katika kifungu ulichopewa. Sasa tafuta jibu lake katika fumbo la maneno uliyopewa. Utapata jibu lake kwa kusoma ukienda chini, kulia au kutoka kwa pembe moja hadi pembe nyingine. Sasa chora mviringo kwa neno hilo. Umepewa jibu la kwanza kama mfano wa kukuonyesha jinsi ya kufanya.

G	K	A	A	H	L	M	I	A
M	A	D	H	A	B	A	H	U
A	R	A	A	C	T	N	X	O
E	M	B	B	B	A	A	L	I
I	E	U	U	V	Z	B	Q	P
Y	L	L	Z	A	W	I	A	B
F	I	Q	I	T	G	I	J	H
M	T	Y	K	Y	T	S	A	R
O	N	P	L	O	A	U	C	V

1. Soma 1 Wafalme 18:1. Je! Mungu alinena na nani? Jina lake linaanza na herufi E.
2. Soma 1 Wafalme 18:2. Je! ni mfalme yupi aliyemchukia Eliya? Jina lake linaanza na herufi A.
3. Soma 1 Wafalme 18:20. Je! Eliya aliwaambia watu wakutane kwa mlima upi? Jina lake linaanza na herufi K.
4. Soma 1 Wafalme 18:22-24. Je! manabii wake waliuhudumia muungu upi? Jina lake linaanza na herufi B.
5. Soma 1 Wafalme 18:25. Je! viongozi hawa wa kidini wa uongo waliitwaje? Jina lao linaanza na herufi M.
6. Soma 1 Wafalme 18:30. Je! mahali ambapo Eliya alijenga, pa kutolea sadaka ya kuteketezwa paliitwaje? Jina lake linaanza na herufi M.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mimi ni wa kwanza na mimi ni wa mwisho. Zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 44:6b).

Sema: Mmejifunza kwamba tatizo moja kubwa lililokuwepo katika Israeli wakati wa Eliya ni kutokuwa na uaminifu katika ibada. Watu wa Mungu walikubali kuiga ibada ya wasiomjua Mungu. Nao wakaanza kuabudu sanamu. Eliya aliwaambia kwamba wakati umefika ambao ni lazima watu wachague mungu ambaye wangemwabudu. Eliya alikuwa na sababu nyingi ambazo zingemfanya aogope kusema hivyo, lakini Mungu alimpa ujasiri wa kusema yote.

Waongoze wanafunzi katika kurudia kifungu cha kukumbuka.

Uliza: Je! ni nani anayezungumza katika kifungu hiki? (Mungu)

Uliza: Je! mnaweza kukumbuka amri ambayo inatuambia yule tupaswaye kumwabudu? (Tazama Kutoka 20:3-6)

Wasaidie wanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa katika kifungu cha kukumbuka iwapo hawajafanya hivyo. Majibu yake yapo hapa chini.

Kifungu chako cha kukumbuka kimeandikwa hapo chini bila herufi kadhaa. Andika herufi zilizoachwa mahali panapotakikana na ukamilishe usemi huu wa Mungu.

MIMI NI WA KWANZA NA MIMI
NI WA MWISHO, ZAIDI YANGU
MIMI HAPANA MUNGU. Isaya
44:6b

WAKATI WA MWISHO

Sema: Tumeona jinsi Eliya alivyokuwa nabii wa ujasiri. Je! ungekuwa Eliya? Je! unaujasiri wa kuweza kuzungumzia uovu ulioko siku hizi? Taja wakati ambapo unahitaji kufanya hivyo. (Wape wanafunzi muda wa kujibu swali hili. Lakini, utapaswa kusema wakati ambapo wanahitaji ujasiri wa kutetea yaliyo ya kweli ikiwa hawatasema cho chote.)

Sema: Eliya alikuwa na ujasiri kwa sababu alimwamini Mungu. Kuna wakati mwingi ambapo Wakristo huhitaji kuwa na ujasiri. Mungu atatupa ujasiri wa kumsimamia kwa valiyo ya kweli iwapo tutamwamini.

AMOSI AHUBIRI JUU YA HUKUMU YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Amosi 1:1-2; 2:4-8; 8:11-12

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wako! Vijana wengi ambao wamehudhuria ibada za kanisa mara kwa mara wamesikia habari za upendo wa Mungu zikisemwa mara nyingi. Upendo wa Mungu u katikati ya imani ya Mkristo. Wanafunzi wako wanapaswa kuwa na uhakika wa upendo wa Mungu. Wanapaswa pia kujua kwamba Mungu ni Mungu wa haki. Mungu hapuuzi maovu. Hawezi kupuuzi dhambi au maovu kwa sababu yu mkamilifu.

Kiini cha somo hili lihusulo nabii Amosi ni hukumu. Mungu alimtuma nabii Amosi kwa watu wa Israeli ili awaonyeshe jinsi walivyokuwa wamekosa kutii na kuwaambia watubu. Alihubiri kwamba Mungu mwenye haki atahukumu kutotii kwao.

Utapaswa kuwasaidia wanafunzi wako wamwelewe Amosi na ujumbe wake. Utapaswa pia kuwasaidia waelewe maana ya ujumbe huu maishani mwao.

SOMA MAANDIKO

Anza kujitayarisha kwa kusoma kitabu chote cha Amosi. Halafu usome kwa makini vifungu vya somo hili.

Amosi amejulishwa kwa msomaji katika Amosi 1:1. Jina hili "Amosi" linamaanisha "kulemewa". Jina hili lilimfaa sana nabii huyu. Alilemewa na mzigo mzito moyoni mwake kwa

sababu ya maovu aliyoyaona maishani mwa watu wake. Alibeba mzigo wa ujumbe moyoni mwake. Huu ulikuwa ujumbe wa hukumu ambao alilazimika awaambie watu aliowapenda.

Amosi hakuwa na uchumi wa unabii. Alikuwa hasa mkulima. Alikuwa pia mchungaji wa kondoo. (Amosi 1:1) Amosi alikuwa pia mtunza mikuyu (Amosi 7:14). Mti wa mkuyu unaweza kufanana aina ya mti uitwao mtini ambao unakua sana katika bara la Afrika. Mtu alipaswa kuminya tunda lake ili liweze kuiva.

Amosi aliishi katika mji uitwao Tekoa. Mji wa Tekoa ulikuwa katika Yuda, karibu kilomita kumi kusini mwa Yerusalemu. Arthi yake ilikuwa kavu na yenye mawe mengi. Maisha hayakuwa rahisi kwa mkulima aliyeishi Tekoa.

Mungu alimwita mkulima huyu kuwa nabii. Amosi alihubiri kati ya mwaka wa 760 hadi 746 B.C. Wanafunzi wengi waliosoma Biblia wanasema kwamba alihubiri kutoka 760 hadi 753 B.C.

Ujumbe wa Amosi ulikuwa ujumbe wa hukumu, na kutaka kufanywe haki. Alizungumzia sana ukatili na kutotenda haki popote alioona mambo haya. Alizungumzia sana jinsi matajiri wanavyowadanganya maskini. Alinenea uhongaji na dhambi ya usherati. Hakuacha kusema kwamba kulikuwa na udanganyifu hata mahali pa kufanyia ibada. Walizifanya desturi

za ibada kuwa za muhimu sana kuliko Mungu.

Amosi alitwa ili kuhubiria Ufalme wa kaskazini mwa Israeli. Hata hivyo, alianza ujumbe wake kwa kulaumu mataifa yaliyo jirani ya Israeli. (Amosi 1:3-2:5) Alitaja mataifa saba, pamoja na Yuda. Watu wa Israeli walipokea mahubiri haya kwa furaha. Hata hivyo, mawazo yao yalibadilika wakati Amosi alipotoa hukumu ya mwisho ya Mungu. Alimalizia kwa kuzungumzia juu ya Israeli. Sehemu inayobaki ya kitabu cha Amosi inalaani Israeli kwa sababu ya dhambi walizomfanyia Mungu.

Tazama zile dhambi ambazo Amosi anataja katika Amosi 2:4-8. Yuda ilikosa kutii mafundisho ya Mungu na walikuwa wakiabudu sanamu. Israeli ilikuwa imewauza waliokuwa utumwani ili kulipa madeni yao. Hawakuwajali walio wadhaifu, maskini wala wasiojiweza. Walikuwa na hatia ya dhambi ya uasherati na wakafanyia ibada mzaha.

Nabii huyu alizungumza kuhusu kile ambacho kingetokea kwa sababu ya dhambi ya Israeli katika Amosi 8:1-12. Alikuwa akizungumza juu ya njaa ya kiroho. Njaa ya kiroho ni sawa na njaa ya ukosefu wa mkate na maji. Mungu ndiye chanzo cha ukweli jinsi alivyo pia chanzo cha chakula. Mungu ndiye aliyesema na Musa, na pia Amosi. Kungekuwa na njaa ya ukweli kama Mungu angekataa kutoa neno lake.

Watu wa Israeli walikuwa wakiamini kulindwa na jeshi lao pamoja na sadaka za kuteketezwa walizotoa. Walikuwa wamekataa kuisikiliza sauti ya Mungu. Sasa, wangepoteza nafasi yao ya

kuisikiliza. Amosi alisema kwamba wakati unakuja ambao wale waliokataa kuisikiliza hawataweza tena kusikia neno la Bwana.

Hata ingawa kitabu hiki kinakazia sana hukumu ya Mungu kwa mataifa mengi hakiwaachi watu bila kuwa na tumaini. Vifungu vitano vya mwisho vinazungumza juu ya tumaini na ahadi inayotolewa kwa watu hao (9:11-15). Aliwasihi watu hao kuacha, "hukumu itelemke kama maji, na haki kama maji makuu" (5:24).

Kusudi la somo hili *kuwasaidia wanafunzi kuelewa ujumbe wa Amosi wa hukumu na kuchunguza maisha yao ili waone mambo ambayo yanaweza kuwafanya wahukumiwe na Mungu.*

KULIFUNDISHA SOMO

Utapaswa kupata wakati wa wiki hii, habari kutoka magazetini zinazoeleza maovu yaliyotendwa nchini. Zinaweza kuwa habari za uhongaji, kuibia maskini, kuiba pesa za kampuni na visa vingine. Waonyeshe wanafunzi wako habari hii na uwaambie kwamba baadhi ya dhambi hizi zilitendwa na watu walioishi wakati wa Amosi.

Uliza: Je! mnafikiri Mungu huudhishwa sana na dhambi ambazo zinatendwa na watu siku hizi? (Ngojea majibu)

Sema: Ndiyo, aliudhishwa na dhambi zilizotendwa hapo zamani na yungali akiudhishwa na za siku hizi. Amosi alikuwa nabii aliyeitwa na Mungu ili awaambie watu wa Israeli jinsi Mungu angehukumu dhambi za. Leo tutajifunza kama kwamba watu wa wakati wa Amosi walikuwa na redio.

Hebu tujifanye kama kwamba mwandishi wa habari ametoka Afrika na kwenda Yerusalemu kupata habari juu ya Amosi na yale anayohubiri.

Wachague wanafunzi wanne ambao ni wasomaji hodari ili waweze kusoma mazungumzo yaliyoko katika somo lao. Mmoja atasoma sehemu ya "mwandishi". Watatu kati yao wanaweza kusoma sehemu za mtu, Rachel, na Amosi. Wahimize ili wasome vizuri na kuelewa. Waambie wanafunzi wengine wasikilize kwa makini. Kazi hii itachukua muda mwingi wa kufundisha, lakini itakuwa ya kuvutia sana kuliko kuwaambia tu ukweli huu.

Utapaswa kurudia tena na kuwaambia mahali ambapo Amosi aliishi na wakati alipohubiri baada ya wanafunzi kumaliza kusoma mazungumzo hayo. Tumia ramani na orodha uliyopewa.

Uliza kama kuna swali lo lote juu ya mazungumzo hayo. Hakikisha kwamba wanafunzi hao wameelewa jinsi hali ilivyo kati ya Yuda na Israeli. Eleza kwamba hata ingawa Mungu aliwapenda watu wake, na yungali anatupenda hata sasa, hawezi kuacha wala kupuza dhambi. Watu wa Israeli walijitea wenyewe hukumu ya Mungu. Sisi hujitea hukumu ya Mungu tunapokosa kumtii hata ingawa tunajua yaliyo mema ya kufanya.

KAZI YA KUFANYA

Wanafunzi wako hupenda kufanya kazi kwa mikono yao. Hupenda kushindana. Hupenda kukariri majibu ya maswali muhimu. Hata hivyo, unaweza kupata shida ya kuwafanya

wafikirie maana ya ukweli huu katika maisha yao. Sehemu moja ya kazi ya somo hili itawasaidia wanafunzi wako kukumbuka ukweli wa maisha ya Amosi. Sehemu inayobakia itawafanya wafikirie maana ya ukweli huu maishani mwao. Wahimize vijana hawa ili waweze kufikiria. Usiwaache wawe wavivu wa akili. Pengine wanaweza kupata shida ya kuandika juu ya yale ambayo Amosi angewaambia vijana wa siku hizi, lakini unapaswa kuwatia moyo waandike.

Mungu alimwita Amosi ili atangaze dhambi za Israeli. Alitaja pia baadhi ya dhambi za watu wake wa Yuda. Soma Amosi 2:4-8 na uandike orodha ya dhambi za Yuda na Israeli katika maneno yako mwenyewe.

DHAMBI ZA YUDA

Walidharau mafundisho ya Mungu

Hawakutii amri za Mungu.

Waliabudu miungu na sanamu.

DHAMBI ZA ISRAELI

Waliwauza utumwani wale waliokuwa waaminifu ambao walishindwa kulipa madeni yao.

Hawakuwajali walio wadhaifu, maskini wala wasiojiweza. Walifanya dhambi ya uasherati.

Waliwaibia maskini.

Waliifanyia ibada mzaha.

Tumia kazi ifuatayo kulinganisha ujumbe wa Amosi na maisha ya siku hizi. Waambie wanafunzi kadhaa wasome yale waliyoandika na mjadiliane juu ya mawazo yao. Amosi angekuwa na ujumbe kama ule aliowaambia Waisraeli, ikiwa angewazungumzia vijana wa nchi hii yetu. Andika katika nafasi ifuatayo yale ambayo unadhani kwamba yangekuwa ujumbe wa Amosi iwapo angekuwa yungali hai.

Soma Amosi 8:11-12. Vifungu hivi vinatoa mfano jinsi mambo yangekuwa kwa watu wa Israeli iwapo hawangetubu. Chora mfano wa picha ambazo zinasimuliwa katika Amosi 8:11-12 katika nafasi ifuatayo.

Utapaswa kuwapa wanafunzi wako karatasi za kuchora picha walizoulizwa iwapo hawatakuwa na nafasi ya kutosha katika masomo yao.

Kamilisha fungu la maneno lililoko upande wa kushoto na maelezo yaliyoko upande wa kulia kwa kuandika herufi ifaayo katika nafasi iliyoachwa.

- | | |
|---------------------------------------|---------------------------------------|
| <u>e</u> 1. Tekoa | a. Miaka ya huduma ya Amosi |
| <u>c</u> 2. Yuda | |
| <u>f</u> 3. Israeli | b. Kazi ya Amosi kabla ya kuwa nabii. |
| <u>b</u> 4. Mchungaji na mkuza mitini | c. Ufalme wa Kusini. |
| <u>d</u> 5. Hukumu | d. Matokeo ya kumkataa Mungu |
| <u>a</u> 6. 760-753 B.C. | e. Mji wa nyumbani kwa Amosi |
| | f. Ufalme wa kaskazini |

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Tafuteni mema, wala si mabaya, mpate kuishi, hivyo Bwana, Mungu wa majeshi, atakuwa pamoja nanyi, kama msemavyo” (Amosi 5:14).

Sema: Amosi alihubiri juu ya hukumu ya Mungu, lakini aliwapa pia watu hao tumaini. Alikuwa na ujasiri wa kusema na kulaumu uovu. Alikuwa tayari kutoa njia ya wema ipatikanayo katika kumtafuta Mungu. Tunajua tofauti kati ya mema na mabaya kwa sababu Mungu mwenyewe ametuonyesha tofauti hii. Sisi hujaribu kufanya mema tunapojua kilichochema. Lakini hatuwezi kutenda mema bila kusaidiwa na Mungu. Kifungu chetu cha kukumbuka kinatuhidi kwamba Bwana atatusaidia iwapo tunataka kufanya yaliyomema.

Waongeze wanafunzi wako kukariri kifungu hiki, bila kukisoma.

WAKATI WA MWISHO

Hebu tazama tena kusudi lako la somo hili. Ulipaswa kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa ujumbe wa Amosi uhusuo hukumu. Ulitakiwa pia kuwasaidia wanafunzi wako kutaja mambo yaliyo maishani mwao ambayo yanaweza kumfanya Mungu awahukumu. Wasaidie kufanya hivyo kwa kuwauliza maswali kama haya: Je! Wewe huwa unadanganyana shuleni? Je! huwa unawachekelea wale ambao hawavai vizuri kama wewe? Je! wewe huwa unacheza michezo kwa kuwakasirisha wenzako?

Maliza mafunzo yako kwa maombi. Pengine baadhi ya wanafunzi wako watataka kukiri mbele ya wenzao makosa waliyofanya. Wahakikishie kwamba Mungu yu tayari kuwasamehe.

HOSEA ANAELEZA UPENDO WA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Hosea 11:1-4;
14:1-4

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wako. Vijana wengi huwa hawajiamini wenyewe na uhusiano wao na wenzao. Huwa wana mashaka mara kwa mara juu ya uhusiano wao na Mungu. Kwa hivyo, wanapaswa kuhakikishiwa kwamba Mungu anawapenda na anaweza kuwasamehe.

Somo hili la Hosea linaweza kuwakumbusha wanafunzi hao juu ya ukuu wa upendo wa Mungu. Litawasaidia kujua kwamba Mungu yuko tayari kusamehe dhambi.

Wanafunzi wako wanapaswa pia kukumbushwa juu ya wajibu wao. Ni lazima wawe tayari kukubali dhambi zao. Wanapaswa kuambiwa kwamba wanatakiwa kukubali makosa yao ili wapate msamaha wa Mungu.

Vijana wengi huona haya kukubali wazi dhambi zao. Hufikiri kwamba dhambi zao ni mbaya sana hata Mungu hawezi kuwasamehe. Wanafunzi hawa wanapaswa kufundishwa kwamba upendo na msamaha wa Mungu ni mkuu sana kuliko dhambi zao.

Wanafunzi wako wanapaswa pia kujua kwamba Mungu hachukulii dhambi kama jambo rahisi. Alisikitikia sana dhambi za Israeli. Dhambi zetu pia humsikitisha Mungu.

Soma Maandiko. Kitabu cha Hosea kimeandikwa kutokana na kuvunjika kwa ndoa kati ya Hosea na Gomeri.

Uhusiano wao unaonyesha jinsi uhusiano wa Mungu ulivyo na Israeli. Israeli wangemfuata Mungu kwa muda mfupi, halafu baadaye kidogo wangeacha kumtii. Mungu aliipenda Israeli hata walipokosa kumtii.

Hosea aliishi katika ufalme wa kaskazini mwa Israeli. Yeye alihubiri huko wakati Isaya alipokuwa akihubiri katika ufalme wa Kusini. Mungu alimtumia Hosea kusema na watu wake kuanzia mwaka wa 748 B.C. hadi 722 B.C.

Soma sehemu utakayoweza ya kitabu cha Hosea. Hakikisha kwamba umesoma pia sehemu ya Sura ya 11 hadi 14. Sasa soma somo la wanafunzi.

Hosea 11:1-4 inalinganisha upendo wa Mungu kwa Israeli na ule wa baba na mwanawe. Mungu alionyesha kwanza upendo wake kwa Israeli alipowaita watu wake kutoka utumwani kule Misri hadi kwenda katika nchi ambapo wangekuwa huru. Lakini wao walipuza upendo wa Mungu. Waliasi na wakakataa kutii. Walimtolea Baali sadaka na wakazifukizia uvumba sanamu.

Israeli ilikuwa ikiitwa kwa baadhi ya makabila yalikuwa upande wa kaskazini na kusini. Yuda ndilo lililokuwa kabila kubwa upande wa kusini. Efraimu nalo lilikuwa kabila kubwa la upande wa kaskazini. Tunaweza kulifikiria jina la Efraimu kama jina la awali la Israeli au Ufalme wa Kaskazini.

Picha hii inaonekana kama inabadilika katika kifungu cha 4 kutoka kwa mtoto hadi kwa ng'ombe dume. Mwenye ng'ombe huwa anaibembeleza sana. Anatumia "mafungu ya upendo" kwa kuifundisha badala ya kutumia fimbo. Hii ni njia nyingine ya kuonyesha neema na wema wa Mungu kwa Israeli.

Hosea 14:1-4. Katika sura hii ya 14, nabii Hosea anazungumza juu ya mambo matatu ambayo ni muhimu kwa kuleta uhusiano mwema kati ya Mungu na watu wake. Nayo ni kutubu, msamaha na uaminifu.

Sura hii inaanza na neno "mrudie Bwana". Waebrania walitumia neno hili kumaanisha toba ya kweli. Ni lazima Israeli waache maisha yao ya kutotii na wamrudie Mungu na kuishi kama yeye.

Kifungu cha 2 kinaanza na maneno haya, "Chukueni maneno pamoja nanyi." Israeli ilitakiwa iseme jinsi watu wake walivyotenda dhambi. Toba si jambo la kuwaza moyoni tu. Ni lazima liwe dhahiri. Hosea aliiambia Israeli watubu dhambi zake kwa Mungu, na wamwombe aondoe ubaya wote maishani mwao, ili wapokee yaliyomema.

Tumeshajifunza kwamba Israeli walitegemea nguvu zao za kijeshi na sanamu badala ya Mungu. Hosea anawaambia katika kifungu cha 3 kwamba ni lazima wamtegemea Mungu tu.

Halafu, katika kifungu cha 4, tunaona kuwepo kwa msamaha. Mungu anaahidi kuwaponya katika uaminifu wao. Hakuna mipaka kwa

msamaha wa dhambi. Anasema kwamba, "Nitawapenda kwa ukunjufu wa moyo." Yungali anatuahidi upendo ule ule.

Andika kazi ifuatayo kwenye karatasi tatu tofauti. Acha nafasi ya kutosha ya kuandika majibu yake. Utapaswa kuzigawa kati ya makundi matatu ya wanafunzi ili waifanye wakati wa darasa. Kazi yenyewe ni hii:

Kundi la 1: Tumieni Biblia zenu na habari za somo hili kutafuta ukweli wote ulioandikwa juu ya maisha ya Hosea na kazi yake. (Mahali alipoishi na kuhubiri, habari za jamaa yake, n.k.) Mwe tayari kutoa ripoti yenu darasani.

Kundi la 2: Someni Hosea 11:1-4. Je! Hosea alinganisha uhusiano wa Mungu na Israeli na nini? Je! alifanyaje hivyo? Andikeni majibu ya maswali haya. Mwe tayari kutoa ripoti yenu darasani.

Kundi la 3: Someni Hosea 14:1-4. Je! Mungu aliwaambia nini watu wa Israeli? Je! Mungu atafanyaje baadaye? Mwe tayari kutoa ripoti ya majibu yenu darasani.

Kusudi la somo hili *kuwahakikishia wanafunzi kwamba Mungu anawapenda na yuko tayari kuwasamehe wakati wa wote wanapokubali wamekosa na kutubu.*

KULIFUNDISHA SOMO

Simulia au wasomee mazungumzo yaliyoko baina ya Maria na Prisila ambayo yako mwanzoni mwa somo la wanafunzi.

Uliza: Je! umewahi kumwomba mtu msamaha lakini yeye akakataa

kukusamehe? (Wape muda wa kujadiliana)

Uliza: Je! mnafikiri nia ya Mungu kwa makosa yetu ni kama ile ambayo Prisila alikuwa nayo juu ya Maria?

Sema: Leo tutajifunza kutoka kwa somo letu la Hosea kwamba itiko la Mungu ni tofauti sana na lile la Prisila.

Wagawe wanafunzi wako katika makundi matatu. Mpe mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kikundi kalamu na karatasi ambayo umeandika kazi itakayofanywa na kundi hilo. Waeleze kwamba unataka wanafunzi wa kila kundi kushirikiana katika majibu ya maswali waliyopewa. Waambie kwamba wana muda wa dakika saba za kufanyia kazi hiyo. Halafu wataulizwa kutoa ripoti ya majibu yao darasani. Yule mwanafunzi aliyepewa kazi hiyo anapaswa kuwaelezea wenzake inahusu nini na awahimiza washiriki wote kusaidia katika kutafuta majibu. Mwanafunzi huyu ndiye atakayetoa ripoti ya kikundi chake.

Watie wanafunzi hao pamoja wakati watakapoonekana kama wamemaliza kazi yao. Mwambie kiongozi wa kundi la 1, kulisomea darasa maswali aliyopewa na kusoma pia majibu yake au kusema kwa maneno yake mwenyewe. Ikiwa kundi hilo limeshindwa kupata ukweli uhusuo maisha ya Hosea, utapaswa kuwasaidia kwa kuwaambia majibu yake.

Waite wanafunzi hao pamoja wakati kwa kuwaambia majibu yake. Tumia ramani iliyoko kitabuni mwako kwa kuwaonyesha mahali Israeli ilipo, yaani ufalme wa kaskazini. Tumia orodha ya

miaka uliyoandika kwa kuelezea wakati ambapo Hosea alihubiri.

Endelea na kundi la pili jinsi ulivyofanya na kundi la 1. Utapaswa kuongezea majibu kwa kueleza maana ya Hosea 11:1-4. Tumia maelezo yaliyoko katika sehemu ya "kujiandaa kufundisha" na katika vitabu vya wanafunzi kwa kufundisha.

Mwishowe, uliza kundi la tatu kutoa ripoti yake. Toa muhtasari wa maana ya Hosea 14:1-4.

Anza mara moja sehemu ya "kazi ya kufanya" na uwasaidie wanafunzi ambao wana shida ya kujibu maswali hayo.

KAZI YA KUFANYA

1. Hosea alikuwa nabii wa Ufalme wa Kaskazini.
2. Mkewe Hosea alikuwa akiitwa Gomeri.
3. Israeli ilitenda kama mtoto aliyeasi na kukosa kutii.
4. Mungu aliwapenda Israeli bila kutojali dhambi zao.
5. Ni lazima Israeli wamrudie Bwana ili Mungu aweze kuwasamehe.

(mtoto, Gomeri, wamrudie, Ufalme wa Kaskazini, aliwapenda)

Waongoze wanafunzi katika kusema kifungu cha kukumbuka. Kaza umuhimu wa upendo wa Mungu na nia yake ya kusamehe dhambi. Eleza kwamba msamaha unategemea kutubu kwa kweli.

Huenda wanafunzi wengi wasiwe wamefanya kazi inayofuata katika sehemu ya "kazi ya kufanya." Ikiwa baadhi yao hawajafanya, basi,

utapaswa kuwaongoza katika kukiri kwa kimoyomoyo.

Sema: Kila mmoja anapaswa kunyamaza kwa dakika chache. Zitazame hatua za kukiri zilizoko katika somo lako. Kwanza kabisa, mwombe Mungu akuonyeshe dhambi zilizoko maishani mwako. Halafu fuata kila hatua za maagizo yanayofuata. Usiangalie yale mwenzako anaandika. Kukiri kwako ni kati yako na Mungu.

Hakikisha kwamba wanafunzi hawa wana maagizo waliyopewa mbele yao. Wape muda wa dakika tano za kukiri dhambi zao. Utapaswa kuwaongoza kwa maombi baada ya kumaliza.

Waambie kwamba wanapaswa sana kutupa zile karatasi ambazo wameandika dhambi zao. Hawapaswi kuzikumbuka kwa sababu Mungu hazikumbuki tena. (Pengine utapaswa kuwapa karatasi za kuandikia).

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, na dhambi za sitazikumbuka tena” (Waebrania 8:12).

Hakuna mtu ambaye angemlaumu Mungu iwapo angewaacha watu wake wa Israeli. Wao waliendelea kutomtii, hata ingawa aliwaonya kupitia kwa manabii. Lakini ukweli ni kwamba Mungu hakufa moyo. Aliendelea kutafuta njia za kuweza kuwaonyesha upendo na huruma zake. Mungu alionyesha upendo na huruma zake kwa kuita Israeli kuwa taifa na kuwa mwaminifu kwao hata ingawa walikuwa wametenda dhambi. Mwishowe, wakati ulipotimia, Mungu

aliweza kumtumia Mwanawe, Yesu Kristo, kuja ulimwenguni ili afe kwa ajili ya dhambi za watu wote. Kila mtu ambaye anamjia Kristo kwa moyo wa kutubu atasamehewa.

ISAYA ALIITWA KUTOA HABARI NJEMA

MASOMO YA BIBLIA: 6:1-8; 9:6-7

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! wanafunzi hao wanafurahia masomo haya juu ya manabii? Pengine wanafurahia kujifunza juu ya ukweli wa maisha ya watu hawa. Wasaidie ili waone pia umuhimu wa ujumbe wa manabii hawa kwa watu wa siku hizi. Je! unawasaidia wanafunzi hao kuuhusisha ukweli huu wa Biblia na maisha yao?

Vijana wengi wamewahi kufikiria juu ya kazi ambayo watafanya wakati wamepata kuwa wakubwa. Somo hili litakupa nafasi ya kuweza kuwasaidia wanafunzi wako kufikiria jinsi Mungu anavyotaka kuwatumia kwa wakati huu na wakati ujao. Wanapaswa kuelewa kwamba Mungu anawaita wafuasi wake wote kuwa watumishi wake.

Utapata pia nafasi ya kuweza kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa kwamba ni lazima kwanza mtu amjue Kristo kabla ya kuwaambia wengine Habari Njema za Yesu Kristo. Isaya alimwona Mungu jinsi alivyo alipoenda kuabudu hekaluni. Jambo hili lilimfanya kujiona kuwa ni mwenye dhambi. Baadaye, alikuwa tayari kumtumikia Mungu. Wasaidie wanafunzi hao kulinganisha yale yaliyofanyika kwa Isaya na yale yafanyikayo maishani mwao.

SOMA MAANDIKO

Soma vifungu vya maandiko ya somo hili. Soma pia Isaya 1. Sura hii inatoa

muhtasari wa yale ambayo Mungu aliwaambia watu wake kupitia kwa Isaya. Sasa soma somo la wanafunzi.

Pengine unafahamu sana habari za Isaya 6:1-8. Ni mojawapo kati ya sura zinazojulikana sana kati ya vitabu vyote vya manabii. Kuna habari nyingi juu ya kuitwa kwa Isaya kuliko nabii mwingine ye yote.

Huenda Isaya alikuwa na umri wa miaka ishirini alipoenda kuabudu hekaluni. Ulikuwa wakati wa mwaka wa 742 B.C. Uzia alikuwa amekuwa mfalme kwa muda wa miaka arobaini. Alikuwa amewatawala vyema watu wake. Lakini sasa alikuwa amekufa. Watu hawakujua kile ambacho kingetokea kwa taifa la Yuda.

Isaya alikuwa kijana wakati huu wa Mfalme Uzia. Alikuwa Mfalme wa pekee ambaye Isaya alikuwa akimfahamu. Pengine Isaya aliona hitaji kuu la kumwomba Mungu awaongoze.

Aliona maono yasiyo ya kawaida alipoenda kuabudu hekaluni. Alimwona Mungu kama Mfalme. Uzia alikuwa amekufa, lakini Mungu Yehova alikuwa akitawala.

Maserafi ambayo yametajwa katika kifungu hiki ni aina ya viumbe vya mbinguni. Viumbe hawa hawajatajwa mahali pengine po pote katika Biblia. Walikuwepo ili kumhudumia Bwana.

Isaya alijiona mwenyewe alipoona utukufu wa Mungu. Alijiona kama ambaye si msafi. Isaya hakuona dhambi

zake tu, bali aliona pia hata dhambi za watu wake.

Mungu alitakasa dhambi za Isaya. Hii ilidhihirishwa wakati maserafi walipoleta kaa la moto na kugusa kinywa cha Isaya.

Isaya alisikia mwito wa kumhudumia Mungu baada tu ya kukiri dhambi zake na kutakaswa na Mungu. Alisema kwamba alikuwa tayari kuwa mtumishi wa Mungu.

Soma Isaya 9:6-7. Mungu alimwita Isaya ili awaambie watu wa Yuda jinsi atakavyo hukumu kutokutii kwao. Alimwambia pia awaambie ujumbe wa tumaini. Mungu angewahurumia watu wake. Siku moja angemtuma yule aliyeahidiwa (Masihi) ambaye angewaokoa kutoka katika dhambi zao.

Hivi ndivyo vifungu viwili tu kati ya vifungu vyote vya kitabu cha Isaya ambavyo vinatuambia habari za kuja kwa yule Aliyeahidiwa.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi ili kujua hatua wapaswazo kuchukua ili Mungu aweze kuwatumia kama watumishi wake.*

KULIFUNDISHA SOMO

Andika ubaoni au kwenye karatasi kubwa neno hili ISAYA.

Uliza: Je! mnajua nini kuhusu nabii aitwaye Isaya?

Mpe kila mwanafunzi nafasi ya kuweza kutaja jambo moja ajualo juu ya Isaya. Itakuwa rahisi kwao kujibu ikiwa wameisha soma somo hili. Ikiwa hawajalisoma bado, waambie watafute ukweli huu wa Isaya katika aya ya tatu, nne, na ya tano.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Isaya 6:1. Tumia maelezo yaliyoko katika kitabu cha wanafunzi na sehemu ya kitabu cha "Kujiandaa Kufundisha" kwa kujadiliana maana ya vifungu hivi.

Mwambie mwanafunzi mwingine asome kifungu cha 3 na 4. Waambie wanafunzi wako wajaze nafasi iliyoachwa vitabuni mwao iwapo hawajakamilisha kazi hiyo.

Kuna sentensi sita ambazo hazijakamilishwa. Mhimize kila mmoja atumie Biblia yake kwa kutafuta maneno yaliyosahihi. Jibu swali lo lote ambalo wanaweza kuwa nalo juu ya vifungu hivi. (Majibu ni: 1. juu, 2. hekalu 3. maserafi, 4. serafti, mabawa, uso, miguu, kuruka, 5. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu 6. misingi ya vizingiti, moshi.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Isaya 6:5-8. Jadili yale yaliyomtokea Isaya. Tumia hatua zifuatazo kuelezea yale yaliyompata Isaya akiwa hekaluni.

Hatua 1: Isaya alimwona Mungu kama mfalme na mtawala wa kweli wa ulimwengu. Alielewa jinsi alivyo mkuu na mtakatifu.

Hatua 2: Isaya alijiona mwenyewe jinsi alivyo na dhambi zake.

Hatua 3: Isaya alimwomba Mungu amtakase naye Mungu alimtakasa.

Hatua 4: Isaya aliweza kusikia mwito wa Mungu wa kumtaka mtu wa kusema ujumbe wake baada ya kusamehewa.

Hatua 5: Isaya alielewa kwamba Mungu alikuwa akimwita ili asema ujumbe wake.

Utapaswa sasa uwaambie wanafunzi wako wakamilishe sehemu ya kwanza ya "Kazi ya Kufanya". Utapaswa kuwaelezea vizuri kwa sababu haitakuwa rahisi kwao kufanya hivyo. Wanapaswa kulinganisha yale yaliyompata Isaya na maisha yao wenyewe. Watasaidiwa kufanya hivyo iwapo wataandika majibu yao. Mnaweza kujadiliana majibu haya.

Mwambie mmoja wao asome Isaya 9:6-7.

Sema: Sehemu hii ina baadhi ya ujumbe ambao Mungu alimtaka Isaya awaambie watu. Mungu alimwambia Isaya awakumbushe watu jinsi atakavyowahukumu kwa ajili ya kutotii kwao. Lakini, alimpa pia ujumbe wa matumaini wa kuwaambia watu.

Uliza: Je! Isaya alikuwa akizungumza juu ya nani katika vifungu hivi? (Yule aliyeahidiwa, Yesu)

Waambie wanafunzi hao waandike vizuri herufi za majina ambayo yamepewa huyu aliyeahidiwa. Waweza kusahihisha majibu yao iwapo wameshayaandika vizuri (Majibu yenyewe ni: Mungu mwenye nguvu, Mshauri wa ajabu, Mfalme wa amani, Baba wa milele.)

Sema: Mungu alimwita Isaya ili amtumikie. Sasa, nitawataka mkamilishe fumbo hili la maneno ambalo litaeleza kile ambacho Mungu alimtaka Isaya afanye.

Eleza jinsi ya kukamilisha fumbo hilo la sehemu ya "Kazi ya Kufanya". Jibu lake ni "Mjumbe".

KAZI YA KUFANYA

Hebu fikiria juu ya maono ya Isaya alipokuwa hekaluni. Fikiria jinsi Mungu alivyomwambia na jinsi alivyomjibu. Sasa jifikirie wewe mwenyewe na yale ambayo Mungu anakutaka ufanye.

Hatua ya kwanza: Ndoto au yale Isaya alijifunza kutoka kwa Mungu.

Hatua ya Kwanza: (Andika hapa chini yale unayoelewa juu ya Mungu):

JIBU LA
WANAFUNZI

Hatua ya Pili: Isaya alijiona jinsi alivyo mwenyewe.

Hatua ya Pili: Je! unaweza kujiona jinsi ulivyo wakati unapoelewa ukuu wa Mungu? (Andika hapa chini jinsi ulivyojiona mwenyewe):

JIBU LA
WANAFUNZI

Hatua ya Tatu: Ombi la Isaya kwa Mungu na kusamehewa kwa dhambi zake.

Hatua ya Tatu: (Andika katika nafasi ifuatayo yale uliyofanya juu ya dhambi iliyoko maishani mwako)

JIBU LA
WANAFUNZI

Hatua ya Nne: Isaya alielewa kwamba Mungu alikuwa akimwita mtu wa kunena ujumbe wake.

Hatua ya Nne: (Andika katika nafasi ifuatayo yale unayofikiria Mungu anataka kuwaambia watu wa siku hizi): _____

JIBU LA
WANAFUNZI

Hatua ya Tano: Isaya aliitikia mwito wa Mungu.

Hatua ya Tano: (Eleza katika nafasi ifuatayo yale ambayo unatarajia kufanya kama mjumbe wa Mungu): _____

JIBU LA
WANAFUNZI

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kisha nikasikia sauti ya Bwana, ikisema Nimtume nani, naye ni nani atakaye kwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi" (Isaya 6:8).

Waongoze wanafunzi wako katika kusema kifungu cha kukumbuka. Utapaswa wakati huu kuweka alama kwa jina la yule ambaye anakariri vyema vifungu vya kukumbuka iwapo unaweka rekodi ya wafanyao vizuri.

Turnia Isaya 6:8 kwa kuwasaidia wanafunzi waone wajibu wao wa kuwashuhudia wale ambao hawamjui Kristo. Sisitiza kwamba watu wanawatazama jinsi wanavyoishi. Matendo yao yanaweza kueleza zaidi kuliko maneno yao.

Wafanye vijana hawa wafikirie juu ya kusudi la Mungu kuhusu maisha yao yajayo. Eleza kwamba kila Mkristo ameitwa na Mungu ili kumtumikia.

Mtu mmoja anaweza kumtumikia Mungu kama mkulima, hali mwingine anaweza kumtumikia kama mchungaji wa kanisa. Mhimize kila mwanafunzi kuombea kusudi la Mungu maishani mwake.

Funga kwa maombi.

MIKA ANAELEZA MAHITAJI YA MUNGU

MASOMO YA BIBLIA: Mika 6:1-8
KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wako. Je! wanaelewa yale ambayo Mungu anahitaji kutoka kwa wafuasi wake? Waebrania walioishi wakati wa Mika waliamini kwamba Mungu ange-wabariki tu iwapo watafuata masharti fulani ya ibada. Walikosa kuona kwamba Mungu alitaka upendo na utiifu wao. Walizichukua desturi fulani kuwa za muhimu sana kuliko ushirika wao na Mungu.

Vijana wengi hutaka kupata idhini ya wazazi wao na watu wengine wakubwa. Hutaka kukubaliwa na marafiki zao. Hutaka pia wakubaliwe na Mungu na wawe na ushirika naye. Lakini hawajui jinsi ya kuhusiana naye.

Maandiko ya somo la leo yatawasaidia wanafunzi wako kuona kwamba Mungu anahitaji ushirika naye kuliko kitu kingine cho chote. Dini za kizamani hufundisha kwamba Mungu atambariki mtu ye yote iwapo atafanya jambo linalofaa katika njia nzuri. Hata Wakristo nao hufikiri kwamba huwa wamefanya yote yanayotakiwa nao watabarikiwa iwapo wamebatizwa na pia wanahudhuria ibada za kanisa.

Mika alihubiri kwamba Mungu alimtaka mwanadamu atende haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu mwenyewe. Hii inamaanisha kwamba Mungu anataka kushirikiana na watu wake. Anapo "enenda" na mtu, mtu yule

hutaka kumtii na kuwaonyesha wenzake upendo wa kuwahurumia.

SOMA MAANDIKO

Soma sehemu kubwa ya kitabu cha Mika jinsi uwezavyo. Hakikisha kwamba umesoma sura yote ya sita.

Mika alikuwa mkulima aliyeishi na kuhubiri kule Yuda. Aliishi karibu na mji wa Morashti, ulio karibu na mpaka wa Wafilisti. Mika alihubiri wakati wa siku za mwisho za huduma ya Isaya, mnamo mwaka wa 735 hadi 710 B.C. Isaya aliongea mbele ya mfalme hali ujumbe wa Mika ulikuwa kwa watu wote. Ujumbe wake ulikuwa sawa na ule wa Amosi kwa sababu alikuwa na mengi ya kusema juu ya kutotendana haki. Tofauti ni kwamba Mika alihubiri nyumbani kwake, yaani Yuda. Amosi aliishi Yuda, lakini alihubiri kule Israeli.

Hali ya kule Yuda ilikuwa sawa na ile iliyokuwa Israeli. Viongozi wa serikali na viongozi wa kidini wa Yerusalemu hawakuwa wakimpendeza Mungu. Walikuwa waovu sana. Hawakujali mahitaji ya waliomaskini na wakawapendelea matajiri ambao wangetoa hongo. Viongozi hawa walijishughulisha sana na jinsi ya kupata ujasiri kuliko kutenda yaliyomema na ya haki. Hata walifanya ibada za masingizio tu. Walitii kanuni za ibada bila kuwa na upendo mioyoni mwao. Mika aliwaambia watu juu ya dhambi hizi. Aliwaambia hasa kile ambacho Mungu alihitaji.

Mika alizungumza sana juu ya tabia ya Mungu na yale ambayo anahitaji kutoka kwa watu wake. Mika 6:1-8 ni baadhi ya sehemu zinazojulikana sana za kitabu hiki. Soma somo lililoko kama mfano wa kuwa kotini. Mungu ndiye aliyelea mashtaka nao Waisraeli ndio waliokuwa wameshtakiwa. Milima na vilima ndio waliokuwa hakimu.

Kuna mambo matatu katika habari hii.

1. Mungu aliishtaki Yuda kwa kutokuwa watiifu, kutotenda haki, wakatili na kutokuwa waaminifu katika mambo ya kidini.

2. Watu wa Yuda walidai kamba walikuwa wakitoa sadaka ya kuteketezwa inayofaa, nao walikuwa tayari kutoa zaidi ya hapo.

3. Mungu alidhihirisha wazi kile anachohitaji kutoka kwa watu wake--kuishi kwa haki, upendo wa kweli na kuwatunza wenzao, na kushiriki kwa uaminifu naye.

Watu walikuwa wakifanya kama kwamba maisha yao ya kawaida hayakuwa na uhusiano wo wote na dini yao. Walidhani kwamba ilitosha tu kufuata utaratibu wa dini yao. Mungu alitaka dini yao na maisha yao yaanzie kwa haki.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi kuweza kuamua jinsi watakvayotembea na Mungu.*

KULIFUNDISHA SOMO

Mwambie mwanafunzi mmoja asome mazungumzo yale baina ya Petro na Tom.

Uliza: Je! unawezaje kujibu swali la Tom? Je! mnafikiri Mungu alihitaji nini kutoka kwa wafuasi wake? (Wape muda wa kujadiliana.) Sasa waambie wanafunzi kadhaa kutaja kitu kimoja ambacho Mungu anahitaji kutoka kwao.

Sema: Tunaweza kupata kile ambacho Mungu anahitaji kutoka kwa watu wake wa kusoma Mika 6:1-8.

Tumia dakika chache kwa kuelezea baadhi ya ukweli wa maisha ya Mika--pale alipoishi na kuhubiri, hali ilivyokuwa nchini mwake. N.K.

Uliza: Je! umewahi kuambiwa na wazazi wako yale ambayo watu hufanya wakati mwana kijiji anaposhtakiwa kwa kufanya kosa au wakati mtu anapomlalamikia mwenzake? (Jadili pamoja swali hili.)

Sema: Katika siku za wakati wa Mika mtu ambaye alikuwa na mashtaka (malalamiko) fulani alitakiwa kwenda uwanjani katika lango la mji. Baadaye, wazee waliweza kuitwa ili wasikilize mashtaka hayo, nao wakate shauri lihusulo tatizo hilo. Tunajifunza kutoka kwa vifungu hivi vya Mika mwamba Mungu alikuwa na mashtaka. Yeye hakwenda katika lango la mji na kuwaita wazee wazungumzie, lakini alitumia mtindo huu kuwasaidia watu waelewe ujumbe wake.

Waweza kurudia majibu ya maswali yaliyo na kichwa cha "Aliitwa Kotini" iwapo wanafunzi wamesoma somo hili na kujibu maswali hayo. Ikiwa hawajajibu, basi wape nafasi ya kufanya mambo yafuatayo:

1. Waseme kile ambacho mashtaka ya

Mungu yalihusu 2. wafahamu yale maswali mawili ambayo Mungu aliwauliza watu wake.

Uliza: Je! Mungu aliwafanyia nini watu ambacho kiliwachukiza sana katika kumwitikia? (Tazama kifungu cha 4).

Waambie wanafunzi watazame katika sehemu ya "Kazi ya Kufanya" na waandike vizuri jinsi Mungu alivyofuatisha yale mambo aliyo-wafanyia Waisraeli.

Sema: Mika, katika kifungu cha 6 na 7, alikuwa akiitikia jinsi alivyothani kwamba watu wengi wangeitikia kwa mashtaka ya Mungu.

Utapaswa kuwaambia wanafunzi wako waandike majina ya aina ya sadaka zilizotajwa katika kifungu cha 6 na 7, iwapo hawajakamilisha kazi yao. Jibu swali lo lote ambalo wanalo.

Uliza: Je! Mungu anaihitaji sadaka zipi ikiwa hapendezwi na hizi?

Wape wanafunzi wako muda wa kuandika vizuri maneno ambayo yanasema yale Mungu anahitaji. (Tazama maelezo chini ya sehemu ya "Mashtaka" kutoka kwa kitabu cha wanafunzi.)

Waongoze wanafunzi hao katika kusema kifungu cha kukumbuka.

Jadili juu ya hatua ambazo mtu anapaswa kuzifuata ili "kwenda kwa unyenyekevu na Mungu" jinsi ilivyoelezwa katika kitabu cha wanafunzi. Hakikisha kwamba kila mwanafunzi anaandika yale anayotarajia kufanya kwa ajili ya kila hatua.

Mnaweza kufanya marudio ya kujifunza majina na mahali ambapo

kila nabii aliishi na kuhubiri iwapo mungali na muda wa kutosha.

KAZI YA KUFANYA

Soma tena Mika 6:3-5. Mungu anataja hapa baadhi ya mambo ambayo yalifanyika maishani mwa Israeli ambayo yalionyesha wema na uaminifu wake.

Hapa chini kuna orodha ya mambo ambayo Mungu aliwafanyia Waisraeli. Andika namba katika kila nafasi iliyoachwa ili kufuatanisha jinsi yalivyotendeka, kuanzia tendo la kwanza hadi la mwisho. Namba ya kwanza, yaani 1, imeshaandikwa katika nafasi ifaayo.

9 Daudi alimwua Goliathi katika vita.

2 Yusufu anaiokoa jamaa yake isiangamie kwa sababu ya njaa.

6 Mungu anawapa Waisraeli chakula cha mana kutoka mbinguni.

8 Kuta za mji wa Yeriko zabomoka mbele ya jeshi la Israeli.

4 Mungu aliwapelekea wamisri misiba kumi.

5 Bahari ya chumvi iligawanyika.

10 Sulemani ajenga hekalu kule Yerusalemu.

7 Mungu anawapatia Waisraeli nyama ya kula wakiwa jangwani.

3 Mungu anazungumza na Musa katika kijiti kiwakacho moto.

1 Mungu anafanya agano na Ibrahimu.

Hebu litazame somo la kwanza. Soma ile orodha ambayo inakuonyesha wakati ambapo kila nabii aliishi.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“...na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!” (Mika 6:8).

Kifungu cha kukumbuka kina-kwambia mambo matatu ambayo Mungu anakutaka ufanye. Jambo la tatu ni “kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako.” Hili linaonekana kuwa ni wazo zuri. Je! linamaanisha nini?

Mungu alienenda pamoja na Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni. Hii inamaanisha kwamba wao walishiriki pamoja. Hata ingawa Mungu ni mkuu na mtakatifu, anataka awe na ushirika nasi.

Je! tunaendaje pamoja na Mungu? Hatua ya kwanza ni kukubali mpango wake wa wokovu. Kila mmoja ametenda dhambi. Kila mmoja amejaribu kuenenda katika njia yake mwenyewe. Kuna njia moja tu ambayo unaweza kuanzia kwa kumfuata Mungu. Nayo ni kutubu dhambi zako na kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako.

Hatua ya pili ni kuwa na wakati wa pekee pamoja na Mungu kila siku. Unaweza kusema naye kwa kuomba. Unaweza pia kumsikiliza akizungumza nawe kupitia kwa Roho Mtakatifu wakati uombapo. Mungu huongea nawe pia kupitia kwa Neno lake ambalo ni Biblia. Je! unahitaji kusaidiwa katika mwenendo wako wa kila siku? Mwalimu, utapaswa kuwapa

wanafunzi wako orodha ya mpango wa kuwawezesha kusoma Biblia yote. Waelezee juu ya kitabu kiitwacho *Nifuate*. Tumia masomo yako ya Biblia kila siku ili yakusaidie kwa kusoma na kuelewa Biblia.

Hatua ya tatu ni kuwa mtiifu. Si rahisi kutii. Lakini, Mungu atakupa nguvu za kukuwezesha kuishi jinsi inavyotakikana. Unapaswa tu kumwomba nguvu hizi.

Hebu fikiria hatua hizi tatu na uandike katika nafasi ifuatayo yale ambayo unatarajia kufanya kwa kila mojawapo.

Hatua ya kwanza: _____

Hatua ya pili: _____

Hatua ya tatu: _____

Funga kwa maombi na umwambie kila mmoja aombe kwa sauti anapomwuliza Mungu amsaidie kufanya kitu kimoja ambacho Mungu anamtaka afanye.

NENO LA BWANA LAMJIA SEFANIA

MASOMO YA BIBLIA: Sefania 1:1-6, 12; 3:17-20

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Omba unapoanza kujifunza somo hili. Mwombe Mungu akusaidie kujua njia za kuweza kuwasaidia wanafunzi wako kuweza kutumia ukweli huu maishani mwao.

1. Soma somo lililoko katika kitabu cha mwalimu. Jaribu kuelewa mambo yaliyokuwa yakifanyika Yuda wakati nabii alipokuwa akitoa ujumbe wake. Kulikuwa na uovu, kutojali ukweli na haki, na uabuduji wa sanamu. Watu walikuwa wakifuata njia za uovu wa majirani zao, yaani Ashuru. Hata baadhi yao walianza kuvaa kama wao. Hebu fikiria juu ya mifano iliyoko nchini mwako sasa ambayo ujumbe huu wa manabii utaizungumzia.

2. Tayarisha maswali ambayo wanafunzi hawa watamwuliza nabii huyu na uandike pia majibu yake ambayo atayasoma. Wape wanafunzi tofauti tofauti kazi hii wakati wafikapo darasani.

3. Fanya mpango wa kumvalisha mwanafunzi mmoja nguo kama zile za Sefania. Tumia kitambaa kikubwa cha nguo kama kanzu na kitambaa kingine kidogo cha kufunga kichwani mwake. Tengeneza hati ya kuvingirisha ambayo atashika mikononi mwake. Andika ujumbe ambao atasoma.

Kitabu hiki kiliandikwa na Sefania ambaye jina lake linamaanisha "yule ambaye Mungu amemficha au amemlinda". Alihubiri wakati wa

Mfalme Yosia naye alikuwa wa ukoo mmoja na mfalme.

Sefania hakuogopa kuongea juu ya dhambi za Yuda. Alikuwa mmojawapo wa jamaa ya ufalme, na alisema ujumbe wa Mungu kwa ujasiri. Wale waliosoma Biblia wanasema kwamba Sefania alimfanya Mfalme Yosia kufanya mabadiliko yaliyotokea kule Yuda.

Neno la Mungu, yaani sheria, lilikuwa limepotea kwa muda mrefu. Watu hawakuwa wamesikia likisomwa wala hawakujua mafundisho yake. Lakini kitabu hiki cha thamani kilipatikana wakati wa utawala wa Yosia. Mfalme aliamuru kwamba sheria hizi zisomwe mbele ya watu, nao watii mafundisho yake. Wakati huu ndio Sefania alianza kuhubiri.

SOMA MAANDIKO

Soma sura zote tatu za kitabu cha Yosia. Madokezo yafuatayo yatakusaidia kuelewa yaliyomo.

Sura ya 1 hadi 2:3 (hukumu juu ya Yuda). Sefania alihuzunika sana kuona watu wa Mungu wakiabudu sanamu na miungu mingine. Walimwabudu na hatia ya kuamini utajiri na kufuata desturi za kigeni. Baadhi yao walidhani kwamba Mungu haku-zichukulia dhambi hatua (1:12). Walifanya tu jinsi walivyopenda wala hawakudhani kwamba Mungu angewaadhibu siku moja. Sefania aliwaonya kwamba siku ya Bwana, ambayo ni siku ya hukumu, inakaribia. Aliwasihi watubu wakati wangali na muda wa kufanya hivyo.

Sura ya 2:4-15 (Adhabu za majirani wa Yuda). Nabii huyu alizungumza juu ya dhambi za majirani wa Yuda walioko upande wa mashariki, magharibi, kusini na kaskazini. Kwanza kabisa alizungumzia Gaza na Filisti iliyoko upande wa magharibi. Alitaja miji minne kati ya ile mitano, Gaza, Ashkeloni, Ashdodi, Ekroni.

Pili, alizungumza juu ya Moabu na Amoni walioko upande wa mashariki. Watu walioishi huko walikuwa wa kizazi cha Lutu. Walikuwa watu wa majivuno mengi na ugumu wa miyojo. Moabu na Amoni ingekuwa kama Sodom na Gomora kwa sababu Mungu angewaangamiza. (2:8-11)

Tatu, alizungumza juu ya Kushi (Ethiopia) iliyoko upande wa kusini. Wanafunzi wengi wanafikiria kwamba Kushi inamaanisha Misri. Kulikuwepo na wakati ambapo Kushi na Misri walikuwa na serikali moja. Nabii alisema kwamba Kushi ingeuawa kwa upanga wake. (2:12)

Nne, Sefania alizungumzia sana adui zao, Waashuru. Hili lilikuwa taifa lililokuwepo upande wa kaskazini, wenye mji mkuu uitwao Ninawi. Ashuru ilitenda kama kwamba haikumtaka Mungu. Iliishi bila kujali na haikufuata amri za Mungu. Nchi hii ingekuwa kama jangwa baada ya hukumu ya Mungu. (2:13-15)

Sura ya 3:1-9 (Dhambi ya Yerusalemu). Yerusalemu ulikuwa mji wa Mungu lakini watu wote walikuwa waovu. Viongozi wa kiroho walitumia ofisi zao kwa kujinufaisha wenyewe. Hawakuwa watiifu na walikataa kutubu. (3:1-8)

Vifungu vitano vya mwisho wa sura ya tatu ni tofauti sana kutoka kwa sehemu nyingine ya kitabu hiki. Ujumbe wake hapo mbeleni ulikuwa wa kuwaonya watu kwamba Mungu atawahukumu watu wote. Lakini sasa nabii anahubiri ujumbe wa matumaini. Anawaahidi wale waliowaaminifu kwamba Mungu ni mwaminifu naye atakuwa pamoja nao.

KUSUDI LA SOMO HILI

Kuwasaidia wanafunzi kutambua njia ambazo wanavutiwa na watu ambao hawamjui Bwana na watambue jinsi wawezavyo kukua kiroho.

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! unaamini nini kuhusu Mungu? (Andika majibu yao ubaoni. Baadhi ya majibu yao yanaweza kuwa kwamba Mungu ni Mtakatifu na anatutaka tuwe watakatifu. Yeye ni mwema. Anatupenda na anatutaka tumtii. Mungu hutenda haki naye huadhibu dhambi.)

Uliza: Je! rafiki zako wanaweza kuyatazama maisha yako na wajue kwamba unaamini kuwa Mungu hukutunza na hakutaki utende dhambi? (Wape muda wa kujibu.)

Uliza: Je! ni vigumu kuwa tofauti na kufanya mambo yaliyo ya haki na ya kweli wakati wenzako hawawezi? Nabii Sefania aliishi wakati wa shida. Watu wengi walikuwa wameacha kuto-mwamini na walikuwa wanaishi kama jirani zao waovu, yaani Waashuru. Baadhi yao hawakuamini kwamba Mungu alijali iwapo walitenda dhambi. Sefania alikuwa tayari kuwa tofauti kwa hivyo aliweza kuwaambia watu ujumbe wa Mungu.

Waambie wanafunzi wawili wasome maandiko. Mmoja atapaswa asome Sefania 1:1-6 na kifungu cha 12, na mwingine asome Sefania 3:17-20.

Waambie sasa wanafunzi hao waangalie katika ramani iliyo katika mwisho wa somo lao. Waonyeshe Yerusalemu, Ashuru, Ninawi, Filistia, Moabu, Edomu na Amoni. Yuda, ambako nabii huyu aliishi, kumechorwa mviringo.

Sema: Hebu na tumwulize nabii mwenyewe aseme nasi.

Nabii anasema: (Yule mwanafunzi aliyejivalia kama nabii, Sefania, aingie darasani na aanze kusoma maandiko yaliyoko kwenye hati ya kuviringi-shwa.)

Siku ya Bwana i karibu. Mungu ataihukumu Yuda. Anahatia ya kuabudu sanamu na kuuamini utajiri.

Majirani zako, Gaza, Wafilisti, Moabu, Amoni, Kushi na Ashuru wataadhibiwa bila kuhurumiwa. Baadhi yao wataangamizwa kabisa.

Yerusalemu, ambako ni mahali penu pa kufanyia ibada, hapata rekebishwa kwa ajili ya dhambi zake. Wameasi kwa kutomfuata Bwana. Viongozi wake ni waovu nao si waaminifu. Mungu ataadhibu kutotii kwake. Tubuni na mrudie Bwana wakati mngali na wakati. Siku ya Bwana i karibu wakati ambapo mtahukumiwa kwa ajili ya dhambi zenu.

Sema: Je! mngependa kumwuliza nabii huyu habari za maisha yake na ujumbe wake? (Wanafunzi hawa wataanza kuuliza maswali ambayo umewapatia.) Swali la kwanza: Nabii Sefania, unaweza kutuambia jinsi ulivyoamua kuwa nabii?

(Maneno ambayo ninasema yametoka kwa Bwana si yangu mimi.)

Swali la pili: Umezungumza mara kwa mara juu ya “siku ya Bwana”, Je! hii inamaanisha nini? (Mungu atawahukumu watu wa Yuda kwa ajili ya dhambi zao, na siku hiyo ndiyo inayokaribia.)

Swali la tatu: Je! Yosia alikuwa Mfalme wa aina gani? (Alikuwa mfalme mwema sana ambaye Yuda ilikuwa naye kwa miaka mingi. Baba yake, yaani Mfalme Manase, alikuwa mwovu sana. Aliwaacha watu waabudu miungu mingine, hata nyota na wakajenga mahekalu ya kuabudia sanamu. Lakini Yosia alikuwa tofauti sana. Alifanywa mfalme alipokuwa yungali mdogo sana mwenye umri wa miaka minane. Alianza kufanya mabadiliko alipofika umri wa miaka ishirini. Aliwahimiza watu wamwabudu tena Bwana.)

Swali la nne: Je! ni nini kilichomfanya mfalme huyu afanye mabadiliko kule Yuda? (Amri za Musa zilikuwa zimepotea kwa muda mrefu. Watu hawakuwa wamewahi kuzisikia zikisomwa. Ni wakati huu ambao maandiko haya yalipatikana hekaluni. Mfalme Yosia aliona umuhimu wa watu wake kumrudia tena Mungu wa kweli. Kwa hivyo alitaka Neno la Mungu lisomwe mbele ya watu nao walitii.)

Swali la tano: Je! kwa nini unaonekana kama umekasirika wakati unapotoa ujumbe wako? (Mungu amekasirika kwa ajili ya dhambi za Yuda, na ndiyo sababu hata nami nimekasirika. Watu wangu wamemwasi Mungu ambaye aliwapenda na akawaokoa kutoka utumwani. Mungu

alisema kwamba tunapaswa kuwa watu wake maalum, taifa takatifu. Lakini sasa watu wa Yuda wanatenda na kufanya kama wale ambao hawajamjua Mungu.)

Swali la sita: Je! Mungu atawaadhibu tu watu wa Yuda? (La hasha! hukumu yake ni kwa watu wote. Ujumbe wangu niliopewa na Bwana ulikuwa wa kuzionya hata nchi zilizo jirani ya Yuda.)

Swali la saba: Je! kwa nini ulisema juu ya Yerusalemu pekee wala sio mji mwingine wote? (Yerusalemu ndiyo sehemu kuu ya kumwabudia Mungu wetu. Makuhani na viongozi wa kiroho wamekuwa waovu sana. Wanatumia vyeo vyao vya heshima kwa kupata pesa. Wao wanajivuna sana wala hawamtii Bwana. Ninawaambia watubu kabla ya kufikia siku ya hukumu.)

Swali la nane: Je! ni ujumbe upi ambao ungeweza kutuambia siku hizi. (Nitawaonya tu jinsi nilivyowaonya watu wa Yuda. Hammwabudu Mungu kwa moyo wa kweli wala kutii mafundisho yake. Hamjifunzi neno lake, wala hamwaambii wenzenu kuhusu Mungu wa kweli. Hata nanyi mtadhibiwa iwapo hamtatubu.)

Swali la tisa: Sisi tungali vijana, sasa tumeweza kuwa tofauti? (Baadhi yenu mtakuwa viongozi wa nchi yenu. Mtapaswa kuwa waaminifu katika kusoma na kujifunza Neno la Mungu. Liache likuongoze jinsi ya kuishi na usione haya kuwaambia wengine juu ya ujumbe wake. Kumbukeni yale maneno niliyosema: "Bwana, Mungu wako, yu katikati yako shujaa awezaye

kukuokoa; atakushangilia kwa furaha kuu, atatulia katika upendo wake..." (Sefania 3:17) Bwana atakuwa pamoja nanyi naye atawasaidia kupata nguvu.

Sema: Asante sana nabii Sefania kwa ujumbe wako kwetu. Tutayazingatia sana maneno yako.

KAZI YA KUFANYA

Watu wa Yuda walikuwa wamesahau Neno la Mungu. Nalo lilikuwa limepotea kwa miaka mingi. Lakini lilipopatikana, Mfalme Yosia alitaka lisomwe mbele ya watu nao walitii.

Tunalo Neno la Mungu siku hizi. Ni kitabu chetu kinachotuongoza kujua jinsi ya kuishi. Jibu maswali yafuatayo yanayohusu Neno la Mungu maishani mwako. Yakamilishe kwa kujibu Ndiyo au La.

- Ninasoma Neno la Mungu kila siku.
- Ninasikiliza mahubiri ya Neno la Mungu kila wiki.
- Ninajaribu kukariri kifungu kimoja kipya kila wiki.
- Ninajifunza Neno la Mungu kwa muda wa nusu saa kila wiki.
- Huwa nafikiria kifungu kimoja cha Biblia kila wiki.

Yaache yale uliyojibu La yakuonyeshe jinsi unavyotaka kulifanya Neno la Mungu liwe la muhimu maishani mwako. Sefania aliwaambia watu watubu kwa sababu "siku ya Bwana ilikuwa karibu." Soma vifungu vifuatavyo vya sura ya I na uandike usemi ambao unaeleza siku hii ya hukumu ya Mungu.

Kifungu cha 4: Nitaunyosha mkono wangu juu ya Yuda.

Kifungu cha 7: Bwana ameweka tayari dhabihu.

Kifungu cha 14: Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu.

Kifungu cha 15: Siku ile ni siku ya ghadhabu.

Kifungu cha 15: Siku ya fadhaa na dhiki.

Kifungu cha 15: Siku ya uharibifu na ukiwa.

Andika neno KOSA au SAWA kando ya kila mojawapo ya usemi ufuatao:

a. KOSA Hukumu ya Mungu iliwahusu tu wale walioishi katika mataifa ya kigeni (1:2-3)

b. SAWA Siku ya hukumu ya Mungu kwa watu wake ilikuwa inakaribia (1:6-7)

c. KOSA Yerusalemu hainge- hukumiwa (1:4)

d. SAWA Baadhi yao walisema kwamba, "Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya." (1:21)

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Wala msiifuatishie namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu" (Warumi 12:2).

"Kufuatisha" kunamaanisha kuiga hali na maelekezo na desturi za mwingine. Taja njia moja ambayo unauacha ulimwengu udhihirishe tabia na mazoea yako.

JIBU LA
WANAFUNZI

"Kugeuzwa" inamaanisha kubadili tabia na mwenendo. Mungu anakutaka utende na ufanane na Yesu. Hebu fikiria jambo ambalo utafanya wiki hii ambalo litakufanya ufanane na Yesu. Liandike katika nafasi ifuatayo.

JIBU LA
WANAFUNZI

WAKATI WA MWISHO

Utapaswa kuzungumzia baadhi ya njia ambazo wanafunzi hawa wanaweza kumfanya Mungu awageuze. Ongoza katika maombi yakujitoa kwa kumfuata Mungu kwa moyo wa kweli.

SURA YA NANE

NAHUMU NABII WA MAANGAMIZI

MASOMO YA BIBLIA: Nahumu 1:1-3, 12-14, na 3:5-7


KUJIANDAA KUFUNDISHA

Je! Wanafunzi wako wanaelewa maana ya dhambi na matokeo yake? Je! wanajua kwamba yale wanayojiamulia sasa yatahusu maisha yao yajayo? Je! unajua michezo au urafiki ambao wanao sasa uwezao kuwaletaka matokeo mabaya siku zijazo? Omba kwamba Mungu atakusaidia katika kufundisha

somo hili ili onyo lililotolewa juu ya Ninawi liweze kuwa la maana maishani mwao.

1. Hebu itazame ramani ifuatayo. Tazama uhusiano wa Ashuru, ambayo Ninawi ndiyo mji mkuu, na Yuda. Kumbuka kwamba Ashuru ilitawala mataifa yaliyokuwa yangali madogo nayo ilikuwa yenye nguvu sana. Ashuru nayo ilitenda maovu mengi. Kitabu cha Nahumu kiliandikwa ili kuonya Ninawi na taifa la Ashuru juu ya dhambi zao.

Dunia ya Manabii



Eliya Mtishbi alitoa unabii Israeli.

Amosi, wa Tekoa, alihubiri Israeli.

Hatuji kijiji cha Hosea. Alihubiri Israeli.

Isaya, wa Yerusalemu, alihubiri Uyahudi.

Mika, Mmorashti, alihubiri Uyahudi.

2. Soma kitabu cha Nahumu mara mbili kabla ya kufundisha somo hili. Tumia madokezo yafuatayo ili uweze kuelewa yaliyomo:

Sura ya 1:1-15 Inaeleza ukuu wa Bwana.

Sura ya 2:1-13 Inaeleza kuanguka kwa mji wa Ninawi.

Sura ya 3:1-19 Inaeleza sababu za kuangamizwa kwa Ninawi.

3. Nahumu ni baadhi ya manabii kumi na wawili wadogo wa Agano la Kale. Wanaitwa “manabii wadogo” kwa sababu ya urefu wa vitabu vyao wala si umuhimu wao. Orodha ifuatayo itakusaidia kupata picha kamili ya manabii waliodumu kwa muda mfupi ambao tunajifunza katika somo hili.

Nahumu: Tunajifunza katika Nahumu 1:1 kwamba mwandishi wa kitabu hiki alitoka Elkoshi. Inaaminika kwamba mji huu ulikuwa kule Yuda, lakini hakuna udhibitisho kamili. Jina la Nahumu linamaanisha “mfariji.” Alikuwa nabii wakati ule ambao Sefania na Habakuki walikuwa wakihubiri ujumbe wao uliotoka kwa Mungu. Hata hivyo, Nahumu aliuelekeza ujumbe wake juu ya mji wa Ninawi, hali ujumbe wa Sefania na Habakuki ulikuwa juu ya taifa la Yuda.

Nahumu alikuwa mtunga mashairi, naye aliandika ujumbe wake katika shairi. Kulikuwa na mikazo aina mbili katika ujumbe wake: (1) maneno ya

KUWAELEWA MANABII WADOGO

<u>Nabii</u>	<u>Mwaka wa Huduma Yake</u>	<u>Watu wa kuambiwa Ujumbe Huo</u>	<u>Maana ya Jina la Nabii Huyu</u>	<u>Ujumbe wa Kitabu hicho</u>
HOSEA	755-715 B.C.	ISRAEL	“Wokovu”	Upendo wa Mungu
AMOSI	760-753 B.C.	ISRAELI	“Mwenye kubeba Mzigo”	Israeli inakaribia Kuhukumiwa.
YONA	782-753 B.C.	NINAWI	“Huwa”	Wokovu wa watu wa mataifa.
MIKA	753-700 B.C.	YUDA	“Ni nani anayefanana na Mungu?”	Haki na dhulumu
NAHUMU	664-654 B.C.	NINAWI	“Mfariji”	Kuangamizwa kwa Ninawi.
HABAKUKI	609-605 B.C.	YUDA	“Kukumbatia”	Uhaki utaishi kwa Imani.
SEFANIA	632-628 B.C.	YUDA	“Yehova huficha”	Siku ya Bwana i karibu.
MALAKI	432-424 B.C.	YUDA	“Mtumishi wangu”	Tubuni na mrudie Bwana.

maonyo ya hukumu ya Mungu ambayo ingetolewa juu ya dhambi za Ninawi, (2) maneno ya matumaini juu ya Yuda kwa sababu kuteswa kwao kungeisha.

SOMA MAANDIKO

Karne zaidi ya moja ilikuwa imepita tangu Yona alipowahubiria watu wa Ninawi. Alikuwa amewaambia watu watubu nao walikuwa wametubu. Lakini sasa Ninawi ilikuwa imesahau mwito wake kwa Mungu. Ilikuwa na hatia ya kuabudu miungu mingine na kutumia uwezo wake kwa kuyatesa mataifa yaliyo madogo. Ilikuwa imetumia nguvu zake za kijeshi na utajiri kuyaumiza mataifa mengine. Maovu yaliyotendwa katika mji huu yaliwakilisha taifa lote la Ashuru. Mungu angewaadhibu kwa ajili ya dhambi zao. Mungu alitumia Nahumu kuiambia Ninawi juu ya ujumbe wa kuja kwa hukumu na maangamizi ya Bwana.

Sura ya kwanza inaeleza juu ya ukuu na nguvu za Bwana. Kifungu cha 1 hadi 3, vinaonyesha kwamba Mungu aliipa Ninawi nafasi nyingi za kutubu. Lakini yeye ni Mungu mwenye wivu na hatawaacha wafuasi wake waitumikie pia miungu mingine.

Kuanzia kifungu cha 12-14, tunapata matumaini yaliyotolewa kwa Yuda. Taifa hili lilikuwa limeteswa na Ninawi, lakini likawa huru hivi karibuni. Ninawi ilionekana kuwa yenye nguvu, lakini wakati unakuja ambapo jina lake halitakumbukwa kamwe.

Sura ya pili inaeleza habari za kuanguka kwa Ninawi. Mfano wa simba ulikuwa unapendwa sana na taifa la Ashuru. Katika kifungu cha 11 na 12, jina la simba limetumiwa kwa kuelezea

taifa lenyewe. Katika miaka iliyopita Ashuru ilikuwa imetenda kama simba kwa kuyaangamiza mataifa mengine. Lakini sasa nayo ingeangamizwa.

Sura ya tatu inaeleza habari za uongo wa Ninawi, wizi, uabuduji sanamu na uchawi. Kifungu cha 5 hadi cha 7, vinaifanisha Ninawi na mwanamke anayedharauliwa kwa sababu ya dhambi zake. Ninawi ilijivuna sana wala haikujua hatari iliyokuwa mbele yake. Kwa sasa, hakuna yule ambaye angeisaidia.

Ninawi ilikuwa karibu na Mto Hedekeli. Mnamo mwaka wa 612 B.C. mvua kubwa iliyonyesha iliufanya mto Hedekeli kufurika na kubomoa sehemu ya ukuta wa mji huo. Jambo hili liliwawezesha maadui wake kuuvamia mji huo. Punde si punde mji wa Ninawi uliangamizwa kabisa jinsi Nahumu alivyokuwa amesema.

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi kujua matokeo ya kukosa na kuwahimiza ili kuweza kutubu dhambi zao kila siku na kupata msamaha wa Mungu kupitia kwa Yesu Kristo.*

KULIFUNDISHA SOMO

Andika maswali yafuatayo ubaoni au kwenye karatasi kubwa.

1. Je! nabii ni nani? (Ni yule asemaye ujumbe wa Mungu)
2. Je! ni nini maana ya neno "Nabii?" (Watabiri)
3. Je! kuna tofauti gani kati ya manabii "wakubwa" na manabii "wadodo?" (Inategemea ukubwa wa maandishi ya ujumbe wao.)
4. Je! ni manabii wapi ambao umejifunza habari zao hadi sasa? (Eliya,

Amosi, Hosea, Isaya, Mika, Sefania)
Eleza kwa ufupi hadithi iliyoko kwenye
utangulizi wa somo la wanafunzi.

Uliza: Je! umewahi kufanya
jambo ambalo ulidhani kwamba
halingejulikana? Pengine ulivunja kitu
nyumbani na ukadhani kwamba
hakutakuwa na ushahidi wo wote.
(Wape wanafunzi wako muda wa
kusema jinsi walivyoona maishani.)

Sema: Ujumbe wa nabii Nahumu
ulikuwa tu kama huo. Watu wa Ninawi
walikuwa wanakaribia adhabu ya
dhambi zao. Mungu alikuwa amewapa
muda wa kutubu, hali wao waliendelea
kutenda maovu kama kwamba Mungu
hakuwa anawaona.

Mwambie mwanafunzi mmoja
afungue katika Yona 3:1-10. Wachague
wanafunzi wengine ambao watasikiliza
majibu ya maswali yafuatayo. (Andika
maswali yenyewe ubaoni.)

1. Je! Mungu alimtuma nani kwenda
kuwahubiria watu wa Ninawi?
(kifungu cha 1-3)
2. Je! Ninawi imeelezajwe katika
vifungu hivi? (kifungu cha 3)
3. Je! watu waliitikiaje ujumbe huu?
4. Je! mfalme alifanyaje aliposikia
ujumbe wa mhubiri?
5. Je! Mungu alifanyaje wakati
Ninawi ilipotubu? (kifungu cha 10)
(Mpe kila mmoja muda wa kuweza
kujibu.)

Sema: Zaidi ya miaka mia moja
ilikuwa imepita tangu Yona alipokuwa
amehubiri kule Ninawi, nao watu
wakatubu. Lakini katika miaka
iliyofuatia, Ninawi ilisahau mwito wake
kwa Mungu. Badala yake ilianza

kufanya maovu mengi kuliko hapo
awali. Mungu alikuwa amevumilia
matendo yao na hakuwa amewaadhibu
kwa sababu ya maovu yao. Lakini sasa
Mungu alikuwa tayari kuchukua hatua,
bali kwanza alimtuma nabii
kuwaambia watu yale ambayo
yangewapata.

Mungu alimtumia nabii aitwaye
Nahumu. Habari ya maisha yake
haijulikani sana. Sura ya 1, na kifungu
cha 1 kinatuambia kwamba alikuwa
akitoka Elkoshi naye alipokea ujumbe
wake kupitia kwa maono. Inaaminika
kwamba alikuwa mwenyeji wa Yuda,
nchi mojawapo ambayo ilikuwa
imeteswa na Ninawi.

Uliza: Je! nabii huyu aliwaambiaje
watu ujumbe wake? (Mwambie
mwanafunzi mmoja asome Nahumu
1:1-3). Je! Mungu ameelezwaje katika
vifungu hivi? (Mwenye wivu, hujilipiza
kisasi, hujilipiza kisasi juu ya adui zake,
si mwepesi wa hasira, ana uwezo
mwingi, atawaadhibu wenye hatia.)

Sema: Nahumu aliwataka watu
waelewe kwamba maneno yake
hayakuwa yametoka kwa mwanadamu,
lakini kutoka kwa Mungu mweza na
mjua yote.

Uliza: Je! Mnafikiri kwamba Mungu
alikuwa mwepesi wa kuonyesha hasira
zake juu ya dhambi za Ninawi? (Ndiyo,
kwani zaidi ya miaka mia moja ilikuwa
imepita tangu walipojifunza juu ya
adhabu ya Mungu kwa dhambi.)

Sema: Ninawi, ambao ulikuwa mji
mkuu uliwakilisha dhambi za taifa la
Ashuru. Ashuru ilikuwa imeionea
mataifa madogo yaliyokuwa jirani
yake. Ilikuwa na jeshi kuu na uwezo

mwingi na hapakuwa na taifa lo lote ambalo lingepigana nao. Yale mataifa madogo yaliliogopa na yalijitoa kwake kwa ajili ya nguvu zake.

Mungu alikuwa na ujumbe wa matumaini kwa taifa la Yuda. Soma sura ya 1:12-14.

Uliza: Je! Mungu aliahidi nini Yuda katika vifungu hivi? (Ninawi ingeondolewa, au kuangamizwa na isipate kuwatesa tena. Nira ya nguvu zake ingevunjwa na Yuda ingekuwa huru tena.

Uliza: Je! kifungu cha 14 kinatuambia ni nini kitakachofanyika kwa Ninawi? (Itaangamizwa na hata jina lake halitakumbukwa kamwe.)

Nahumu, katika sura ya 3:5-7 alisema kwamba Ninawi ilikuwa kama kahaba. Dhambi zake zingeonekana na hakuna ambaye angewafariji au kuwasaidia.

Sema: Unabii huu ulitimizwa tu baada ya miaka michache. Hebu tazameni katika ramani yenu pamoja nami na mwone mahali Ninawi ilipo. Mji huu uko karibu na Mto Hedekeli. Historia inaonyesha kwamba mnamo mwaka 612 B.C., mto huu ulifurika na ukabomoa kuta zilizouzunguka mji huu, nao Wakaldayo na Wamede wakauvamia mji huu na kuuangamiza kabisa. Baadaye, mahali ambapo mji huu ulikuwa hapakuweza kutambulikana. Hivyo basi, unabii wa Nahumu ulitimia kweli.

Uliza: Je! kumekuwa na wakati ambapo wazazi wako wamekwambia ufanye kitu au uende mahali fulani, lakini ukasahau walichokwambia? Pengine ulidhani kwamba walikuwa wakikutania. (Wape nafasi ya kuweza kutoa maoni yao.)

Uliza: Je! walifanyaje walipopata habari zako za kutotii?

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Hesabu 32:23. ("...nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi.")

Adhabu si tendo la kwanza la Mungu. Anataka kutufanyia kama Baba mwenye upendo na kutusamehe dhambi zetu. Katika Nahumu 1:13, mshairi anaeleza juu ya kuachiliwa kwa mfungwa au kuokolewa. Hii ni picha ya kweli ionyeshayo jinsi Mungu afanyavyo anapotusamehe.

Uliza: Je! kuna dhambi maishani mwako ambayo unafikiri kwamba Mungu haijui? Je! unadanganya? Je! umewahi kuchukua kitu cha mwenzako bila yeye kujua? Je! wewe huwatii wazazi wala waalimu wako? Je! umewahi kujaribiwa kunywa pombe au kutumia madawa ya kulevya? Hebu inamisha kichwa chako na umwombe Mungu akusamehe. Taja dhambi hiyo wakati unapoomba. (Wape muda wa kuomba kimoyomoyo, halafu umelizie kwa maombi mafupi.)

KAZI YA KUFANYA

Soma Nahumu 1:1-3 na uandike jinsi Mungu atakavyoitendea dhambi:

Kifungu cha 1: "Bwana ni Mungu mwenye wivu, naye hujilipiza kisasi."

Kifungu cha 2: "Bwana hujilipiza kisasi juu ya adui zake."

Kifungu cha 3: "Bwana si mwepesi wa hasira; ana uweza mwingi."

Kifungu cha 36: "...wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe."

Nahumu 1:12-14 ina ujumbe wa maonyo juu ya Ninawi, na ujumbe wa

kufariji juu ya Yuda. Andika herufi N kando ya usemi unaoelezea juu ya Ninawi na herufi Y kando ya usemi unaoelezea juu ya Yuda.

Kifungu cha 12: N "Ijapokuwa wana nguvu zilizo timilifu, ijapokuwa ni wengi, hata hivyo watakatwa, naye atapita na kwenda zake."

Kifungu cha 12: Y "Ingawa nimekutesa, sitakutesa tena."

Kifungu cha 13: N "Na sasa nitavunja nira yake nami nitakupasulia mafungo yako."

Kifungu cha 14: N "Bwana ametoa amri katika habari zako ya kwamba asipandwe tena mtu awaye yote mwenye jina lako."

Kifungu cha 14: N "Nitakufanyia kabui lako; kwa maana u mbovu."

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Bwana ni mwema, ni ngome siku ya taabu; naye huwajua hao wamkimbilia" (Nahumu 1:7).

Kifungu chetu cha kukumbuka kinatuambia mambo matatu yahasuyo Mungu:

1. Yeye ni mwema
2. Yeye ni ngome
3. Yeye ni mahali pa kukimbilia

Waongoze wanafunzi hao katika kusema jinsi Mungu alivyomwema. Halafu zungumza juu ya maana ya "ngome" na "kimbilio". Rudieni kifungu hiki pamoja hadi mtakapo-kifahamu vyema.

WAKATI WA MWISHO

Wakumbushe wanafunzi juu ya ukweli wa somo la leo unaohusu dhambi na matokeo yake. Mungu hajabadilika. Hatatuacha tustarehe bila kuadhibu dhambi zetu. Tunaweza kufikiri kwamba dhambi zetu ni ndogo na Mungu hazioni kamwe. Hii si kweli. Wazo au tendo lo lote ambalo halimpendezi Mungu litaadhibiwa.

Mungu ametoa njia katika Kristo, ya kuweza kusamehe dhambi zetu, lakini ni juu yetu kuzitubu na kuomba msamaha. Waambie wanafunzi hao kutumia kila jioni wiki hii kwa kutubu dhambi zao na kukubali msamaha wa Mungu.

Imbeni pamoja wimbo usemao, "Mungu yu Mwema." Funga kwa maombi ya kumshukuru Mungu kwa wema wake.

HABAKUKI, NABII WA MASWALI

MASOMO YA BIBLIA: Habakuki
1:1-4, 12-14; 2:2-4; 3:17-19

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Vijana huwa na maswali mengi sana. Hujiuliza, kwa nini ni rahisi kwa wanafunzi kadhaa kupita mitihani yao hali wengine husoma kwa bidii lakini wanaanguka? Kwa nini ni rahisi kwa wanafunzi kadhaa kupata nafasi katika shule wanazotaka, lakini wengine hawapati? Mbona kuna wazazi kadhaa wanaoishi pamoja furaha hali wengine wanatengana au kuachana? Kwa nini watu waliowema hupata shida?

Wanafunzi hawa wataweza kutambua hali ya Habakuki. Nabii huyu alimwuliza Mungu maswali, na majibu yake yalikuwa ya muhimu kwake. Yeye hakujibiwa haraka lakini alijifunza kumwamini Mungu hata wakati ambapo hakuelewa. Omba, kwamba wanafunzi wako watamwamini Mungu kwa kutojali hali au matendo ambayo yanawafanya wamwulize Mungu maswali.

Rudia kwa kusoma kitabu cha Habakuki ili uelewe ujumbe wake. Madokezo yafuatayo yatakusaidia.

1. Habakuki 1:1-4, Swali la kwanza la Habakuki: Je! watu wema wa Yuda watateseka kwa muda gani hali waliowaovu wanazidi kuendelea?

2. Habakuki 1:5-11, Jibu la Mungu: Wale wafanyao maovu kule Yuda wataadhibiwa. Wewe ngojea tu, Mungu atawaachukulia hatua. Yeye anajua wakati ulio mwema kwake.

3. Habakuki 1:12-2:1: Swali la Pili la Habakuki: Je! kwa nini Mungu alikuwa akitumia watu waovu kuwaadhibu wale ambao si waovu?

4. Habakuki 2:2-20, Jibu la Mungu: Wakaldayo (au watu wengine wa Babeli) wataadhibiwa lakini walio wa haki wataishi kwa imani.

5. Habakuki 3:1-19, Ombi la Habakuki: Mungu alimkumbusha kwamba yeye ni mkuu na anauwezo wa kuwaadhibu waliowaovu, lakini anajua wakati uliomwema wa kufanya hivyo. Habakuki alimalizia kitabu chake kwa kumshukuru Mungu.

Kuna vifungu vizuri katika kitabu hiki ambavyo unaweza kuvikumbuka. Vitabu yavyo: "...mwenye haki ataishi kwa imani yake." (2:4) "Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari." (2:14) "Lakini Bwana yumo ndani ya hekalu lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele zake." (2:20)

Tunajua machache sana juu ya nabii huyu isipokuwa jina lake. Alitabiri mara tu kabla Yuda haijaletwa vita na Wakaldayo. Huu ulikuwa mwaka wa mwisho wa karne ya saba. Pengine ilitokea wakati wa mwisho wa utawala wa Mfalme Yosia, na mwanzoni wa utawala wa Mfalme Yehoiakimu. Jina la Habakuki linamaanisha "kukumbatia". Aliishi Yuda na alikuwa Mshairi ambaye alitaka kuona haki ikitendwa.

SOMA MAANDIKO

Habakuki aliona kuwepo kwa uovu na dhulumu katika taifa la Yuda. Ilionekana kama kwamba waovu walikuwa wakituzwa, na waliowema walikuwa wakiadhibiwa. Alishangaa kwa nini Mungu aliwaacha wateule wake kutendewa hivyo. Je! haki ya Mungu ilikuwa wapi?

Sura ya 1:1-4: Mbona ni hivyo, Bwana? Habakuki alieleza ujumbe wake kama ule aliouona. Alijua uovu uliokuwa katika nehi yake na ulikuwa mzigo mkubwa kwake. Sheria ya Mungu ilikuwa ikidharauliwa na waliowaovu. Je! hapakuwepo na haki?

Mungu alimjibu kwamba ange-watumia Wakaldayo kuwaadhibu waovu walioko Yuda. Wakaldayo waliishi kusini mwa Babeli. Habakuki alijua kwamba Mungu alikuwa tayari kuihukumu Yuda. Hakuwa akitatizwa na matendo ya Mungu, lakini alitaka kujua wenye haki wangeteseka kwa muda gani.

Sura ya 1:12-14: Je! kwa nini Mungu atawatumia waliowaovu kwa kuwaadhibu wasio waovu? Nabii huyu alijua kwamba watu wake walikuwa waovu. Lakini hakuelewa kwa nini Mungu angewatumia Wakaldayo, waliokuwa waovu, kwa kuwaadhibu.

Sura ya 2:2-4, Jibu la pili la Mungu lilikuwa kwamba Wakaldayo nao wangepadhibiwa, lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake. Habakuki aliambiwa aandike maono aliyoonna, na kuyadhihirisha wazi ili kila mtu aweze kuyaona. Ujumbe huu ulitakiwa uandikwe kwenye vibao. Ulipaswa

uandikwe kwa herufi kubwa ili iwe rahisi kwa mtu apitaye karibu kuweza kusoma. Ujumbe wenyewe ulikuwa kwamba wale wenye haki na waaminifu kwa Mungu watatuzwa hata ingawa kuna maovu mengi. karibu nao. Walipaswa kuishi kwa imani. Mungu alikuwa akitawala hata hawangeweza kuona kilichokuwa kikifanyika.

Sura ya 3:17-19, Imani ndiyo msingi wa tumaini. Sehemu ya kwanza ya sura hii inaonyesha kwamba Habakuki alijua kwamba Mungu alikuwa mwenye nguvu na kujali. Alimtarajia Mungu ashughulikie haki. Sura hii inaishia na ombi la kujitoa kwa Mungu. Hali haikuwa imebadilika, lakini alikuwa na tumaini. Alipata moyo wa kumwamini Mungu, na huu ndio uliokuwa msingi wa tumaini lake. Imani yake haikutegemea yale ambayo aliyaona, lakini juu ya tabia ya Mungu. Kwa hivyo angefurahi katika Bwana. Mungu angekuwa nguvu zake.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi ili waonyeshe matumaini yao katika Mungu hata wakati wa shida maishani mwao.*

KULIFUNDISHA SOMO

Uliza: Je! unaswali ambalo ungependa kumwuliza Mungu? Pengine una tatizo na huelewi kwa nini mambo yanatendeka jinsi hiyo. Je! ungeuliza nini, iwapo ungejua kwamba Mungu alikuwa anataka kukujibu?

Sema: Hebu tazameni katika sehemu ya kazi ya kufanya ya somo lenu. (Waonyeshe wanafunzi hao sehemu ambayo wanapaswa kuandika swali ambalo wangependa kumwuliza

Mungu. Uliza baadhi ya maswali ambayo yatawafanya wafikirie yale waliyonayo na uwape muda wa kuweza kuyaandika.)

Anza kwa mfano ufuatao:

“Kwa nini imefanyika kwangu hali si kwa mtu mwingine ye yote?” Rose alinungunika huku akitupa vitabu vyake sakafuni. Alikuwa akirudi nyumbani wakati wa mvua, nalo basi likapita huku likikanyanga matope yaliyokuwa karibu naye. Matope yale yalimrukia huku yakiichafua vibaya nguo yake mpya. Hakuna mwingine ye yote aliyepatwa na matope yale, ila yeye tu. Je! ni kwa nini?

Uliza: Je! umewahi kujisikia kwamba hasa shida nyingi hutokea kwako tu wala si kwa wengine? (Wape muda wa kuweza kutoa maoni yao.)

Sema: Nabii Habakuki aliuliza swali kama hili miaka mingi iliyopita. Aliishi Yuda wakati wa shida nyingi. Yosia, aliyekuwa mfalme mwema alikuwa amekufa naye Yehoiakimu alikuwa sasa ndiye Mfalme mpya. Wakaldayo, ambao walikuwa sehemu ya milki ya Wababeli, walikuwa wameshinda mataifa yaliyo madogo na walikuwa wakiwatisha kwamba wangewashinda. (Wahimiza wanafunzi hao kupata mahali ambapo Yuda na Babeli iko katika ramani ya “Ulimwengu wa Manabii” ambayo wameitumia katika masomo yaliyopita.) Watu waliowema walikuwa wakiteseka, hali wale waovu walionekana kama wanaendelea vyema. Nabii huyu aliuliza, “Je! Mungu, mbona, ni sisi tu?”

Habakuki alijua kwamba watu wa Yuda hawakuwa watiifu kwa amri za Mungu. Hata kulikuwa na maovu na dhulumu nyingi nchini humo, lakini kulikuwa na baadhi ya watu ambao walibakia waaminifu kwa Mungu. Habakuki alishangaa ni kwa nini Mungu aliacha kuteswa huku kuwepo. Alimwuliza Mungu baadhi ya mambo yaliyomsumbua.

Sema: Hebu fikiria kwamba Habakuki alikuwa akiishi sasa naye mwandishi wa habari ameenda kumhoji nabii huyu. Hebu tazameni katika masomo yenu na mwone jinsi mahojiano hayo yangekuwa. (Mchague mmoja wao kuwa mwandishi wa habari na mwanafunzi mwingine kuwa Habakuki. Anza kwa kuwasomea utangulizi ufuatao: Gazeti la Mataifa ya Biblia, Yuda 606 B.C.)

Uliza: Habakuki alimwendea Mungu na maswali yake. Je! ni vyema kumwuliza Mungu maswali tuliyo-nayo? (Ndiyo, lakini hatupaswi kumlaumu Mungu tunapopatwa na shida. Mungu anatutaka tuwe wavumilivu, jinsi alivyowaambia watu wa Yuda kuwa wavumilivu na wamngojee awajibu.)

Uliza: Mungu alimwambia Habakuki kwamba mwenye haki ataishi kwa imani yake. (Habakuki 2:4) Je! mtu anawezaje kufanya hivi? (Ishi kila siku ukiamini kwama Mungu ndiye mtawala. Mwamini hata ikiwa hakuna ushahidi wa kuthibitisha mabadiliko atoayo. Uwe mwaminifu kwa Mungu katika yote ufanyayo.)

Sema: Tafuteni Habakuki 3:18-19 katika Biblia zenu. (Mwambie

mwanafunzi mmoja asome vifungu hivi.) Nabii huyu alipoandika vifungu hivi, hakuwa amejibiwa na Mungu. Lakini aliamini kwamba Mungu alikuwa akitenda kazi katika Yuda. Alisema kwamba angemfurahia Bwana ambaye alikuwa nguvu zake hata ingawa kulikuwa na shida. Mwambie mwanafunzi mmoja asome kifungu cha 19.

Sema: Kulungu ni kama swala mdogo. Ana miguu ambayo inaweza kupanda hata mahali pasipowezekana, na abakie hapo hapo bila kuanguka. Maana yake kwetu ni kwamba tunaweza kumwamini Mungu hata wakati wa shida naye atatulinda. Atatupa miguu ambayo itatulinda hata wakati wa shida.

Uliza: Je! tunawezaje kuonyesha uaminifu wetu kwa Mungu hata wakati wa shida? (Majibu yao yanaweza kuwa kama haya: Tuamini na tusiwe na shaka kwamba Mungu anatawala. Tuombe. Tuombe Mungu shida zetu na tuamini kwamba atatujibu. Tuwe wavumilivu hata ingawa hatutajibiwa haraka. Waambie wenzako juu ya Mungu "ajuaye yote" na "anayetutunza".

Sema: Hebu tazameni tena swali mliloandika wakati wa mwanzo wa somo hili. Anza sasa kumwamini Mungu kwamba atakujibu. Taja njia moja ambayo unaweza kumwonyesha Mungu uaminifu wako wiki hii kwa kukujibu swali lako.

KAZI YA KUFANYA

A. Soma Habakuki 1:1-4. Andika swali ambalo Habakuki aliuliza kwanza katika maneno yako mwenyewe. Swali la kwanza: Je! watu wema wa Yuda

watateseka mpaka lini hali wale waovu wanaendelea kufanikiwa? Soma Habakuki 1:13 na uandike lile swali la pili ambalo Habakuki aliuliza. Swali la Pili: Je! kwa nini Mungu alikuwa akitumia waliowaovu kwa kuwaadhibu waliowema?

Sasa andika swali ambalo ungependa kumwuliza Mungu. _____

B. Soma Habakuki 2:2-4 na uweke alama hii (✓) kando ya jibu linalosahihi.

1. Jibu la Mungu kwa Habakuki lilikuwa

(a) liwe kama siri.

✓(b) liandikwe vizuri juu ya mbao za mawe.

(c) lisomewe makuhani kule hekaluni.

2. Mungu alisema kwamba jibu lake lingekuwa

(a) halingejulikana.

✓(b) lingetimia.

(c) lingechelewa kwa muda mrefu.

3. Mungu alisema kwamba watu wanapaswa waitikie kwa

✓(a) kuishi kwa imani.

(b) kuwaambia viongozi juu ya shida zao.

(c) kujihurumia wenyewe.

C. Soma Habakuki 3:18-19. Nabii huyu alitikia mwito wa Mungu kwa

kuomba. Andika katika nafasi ifuatayo
jinsi Mungu alivyo kwa Habakuki.

cha 17, na wale wengine kifungu cha 18.
Someni wote pamoja kifungu cha 19.

Imba wimbo usemao, "Mwamini
Mungu" au wimbo wote wote
unaoonyesha imani yetu kwa Mungu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

**"Tazama, roho yake hujivuna,
haina unyogu ndani yake, lakini
mwenye haki ataishi kwa imani
yake" (Habakuki 2:4).**

Andika maelezo mafupi ya maneno
haya matatu yaliyo ya muhimu katika
kifungu hiki.

Haki: (Kuidhinishwa kuwa mwema
mbele ya Mungu) _____

Kuishi: (kuwa na ulinzi, na
uhakikisho na kumwamini Mungu)

Imani: (Kuwa imara, na kuja
kwamba yale Mungu aliyosema
yatafanyika) _____

WAKATI WA MWISHO

Soma pamoja Habakuki 3:17-19
kama ombi lako la mwisho. Nusu ya
wanafunzi watapaswa kusoma kifungu

MPANGO WA MUNGU KWA YEREMIA

MASOMO YA BIBLIA: Yeremia
1:4-10, 18:1-6

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Mfululizo huu wa masomo umekusudiwa kuwasaidia wanafunzi kufahamu mambo ya manabii. Inawabidi wajifunze nabii ni nani, kazi yake na mafunzo yapatikanayo kutokana na maisha na huduma za manabii.

Yeremia alikuwa mmojawapo wa manabii "wakubwa." Kitabu alichoandika ni kimojawapo cha vitabu virefu sana vya manabii. Alihudumia kama nabii kwa muda wa kama miaka hamsini ambao ulikuwa mrefu sana.

Wafikirie wanafunzi wako. Je! wanajifunza ukweli ambao wanaweza kuutumia katika maisha yao? Somo la juma hili linahusu Yeremia lina ukweli ambao wanaweza kutumia maishani mwao. Ukweli huo ni 'kwamba wale waaminio wanapaswa kuwa waitikivu kwa Mungu kama vile udongo ulivyo katika mikono ya mfinyanzi. Jambo hili huhitaji utiifu na uvumilivu hata wakati wa shida.

Utapaswa kufanya vitu hivi unapotayarisha somo lako.

1. Ombea kila mwanafunzi kwa kutaja jina lake kila siku wiki hii.
2. Mwombe Mungu akufundisha njia ya kuwaelezea vizuri wanafunzi kuhusu somo la Yeremia.
3. Jifunze habari za wafinyanzi wa kienyeji ambao wanafunzi wanawafahamu.

4. Panga ili uje darasa na chombo kilichofinyangwa nchini mwako kama mfano wa kuonyesha wanafunzi wako.

5. Soma maandiko yote kwa makini, na usome pia somo la wanafunzi na waalimu.

6. Kusanya vifaa vinavyohitajika kwa somo hili, kalamu, karatasi na udongo.

7. Andika kila neno la kifungu cha kukumbuka katika vipande vya karatasi ambazo zitatumiwa katika kufundisha kifungu hicho.

Yeremia alitoka katika kijiji cha Anatholi, karibu kilomita nane kutoka Yerusalemu. Baba yake Helkia, alikuwa kuhani. (1:1) Yeremia alikuwa ametolewa kwa kazi ya Mungu hata kabla ya kuzaliwa. (1:5) Aliitwa kuwa nabii akiwa yungali mtoto, (1:6) na alitumika kama nabii kwa muda wa miaka hamsini.

Huenda Yeremia alikuwa mtu mpweke sana. Hakuoa wala kuwa na jamaa, na ujumbe wake uliotoka kwa Mungu haukuwa ukipokelewa vizuri na watu. Yeremia alikuwa jasiri na alimtanguliza Mungu mbele ya mahitaji yake yote.

SOMA MAANDIKO

Soma kitabu chote cha Yeremia wiki hii iwapo utaweza. Unaweza ukasaidiwa na madokezo yafuatayo. Tumia muda mwingi katika kusoma sura ya 1 na 18.

1. Yeremia sura ya 1 hadi 20. Yeremia alitoa unabii wakati wa utawala wa Mfalme Yosia. Yeye aliitwa kuwa nabii

na akatabiri kwamba Yerusalemu ingeamizwa na maadui zake. Watu nao wataadhibiwa kwa kutotii kwao. Anaonyesha jinsi Yerusalemu itakavyovunjwa kama udongo mikononi mwa mfinyanzi.

2. Sura ya 21 hadi 39. Yeremia alitabiri wakati wa utawala wa Mfalme Yehoyakimu na Mfalme Zezekia. Anatabiri kuhusu miaka sabini ya kuwa utumwani chini ya Babeli na kuharibiwa kwa hekalu. Anasaidiwa na Baruku kuandika maneno ya Mungu katika kitabu.

3. Sura ya 40 hadi 45. Yeremia anatoa unabii baada ya kuangamizwa kwa Yerusalemu.

4. Sura ya 46 hadi 52. Yeremia anatoa unabii akishutumu mataifa yasiyoamini.

Yeremia 1:4-10. Mungu alikuwa na mpango na Yeremia wa kuwa nabii hata kabla hajazaliwa. Alimwita wakati walipokuwa mtoto, jambo ambalo lilimshangaza sana Yeremia. Mungu alimkemea Yeremia alipoanza kulalamikia umri wake. Mungu alimwahidi kuwa atamwongoza na kumlinda.

Mungu alimwambia Yeremia kwamba alikuwa akimchagua awe juu ya mataifa na hata falme. Jambo hili lingekuwa la kuogopesha kwa kijana ambaye alikuwa akijua uovu wa kutoabudu Mungu katika nchi yake. Kifungu cha 10 kinasema kwamba Yeremia alipaswa ang'oe, na kubomoa, na kuharibu na kuangamiza, ili ajenge na kupanda. Alipewa amri ngumu sana!

Neno la Mungu lilitimia. Watu wa Israeli na Yuda waling'olewa na

kupelekwa katika nchi geni kama mateka. Baadaye, walirudishwa kwao baada ya miaka mingi kupita ili kujenga na kupanda tena.

Yeremia 18:1-6. Vyungu vilikuwa vya muhimu na vilisaidia sana wakati wa Yeremia. Vilitumiwa kwa kuwekea maji, kuhifadhi mafuta, nafaka, matunda na mboga. Kila jamii ilikuwa na mfinyanzi ambaye alikuwa akipata pesa kwa kutengeneza na kuuza vyungu.

Mungu alimwambia Yeremia kwenda nyumbani kwa mfinyanzi. Alipofika huko alimkuta mfinyanzi akitengeneza chombo fulani. Lakini kitu kiliharibu chombo hicho kikiwa mikononi mwa mfinyanzi yule. Mfinyanzi yule hakutupa udongo ule. Badala yake alianza kuufanya upya. Hatimaye alitengeneza chombo alichokikusudia.

Yeremia alijifunza jambo ambalo Mungu alimtaka ajifunze kutokana na kitendo kile. Alitambua kwamba mfinyanzi angefanya vile apendavyo na udongo huo. Udongo huo ulikuwa mali yake. Mungu alikuwa akimwonyesha Yeremia kwamba hivi ndivyo ilivyokuwa na watu wake wa Yuda. Kama vile tatizo lilivyokuwa kwa udongo, wala si mfinyanzi, ndivyo basi tatizo lilivyokuwa la watu wa Yuda kwa kutojii kwao, wala si kwa Mungu mwenye upendo. Mungu angewafanya wawe watu aliotaka wawe, iwapo wao wangemtii. Lakini yeye angeendelea tu kuwaadhibu iwapo wangekataa kumtii na kufanya jinsi watakavyo. Angewafanya kuwa wapya tena.

Kusudi la somo hili ni *kuwatia moyo wanafunzi kuweza kutii Neno la Mungu na mpango wake kwao.*

KULIFUNDISHA SOMO

Waonyeshe wanafunzi hao chombo kilichofinyangwa ulichokuja nacho darasani. Waelezee kuhusu chombo hicho. Wape nafasi ya kuweza kutaja mahali ambapo wanaweza kuona wafinyanzi wakifanyia kazi yao.

Uliza: Je! ni nani aliyewahi kuona mfinyanzi akitengeneza chungu au chombo cho chote kutoka kwa udongo? (Wape wanafunzi nafasi ya kujadiliana vile ambavyo wamewahi kuona. Baadaye, mwambie mwanafunzi mmoja aeleze jinsi udongo ulivyo.)

Sema: Udongo huwa si mzuri kwa kuutazama wakati mfinyanzi anapoanza kuufinyanga. Hali mfinyanzi huweza kuuchukua na kutengeneza chombo ambacho huwa cha muhimu na cha kupendeza.

(Sasa chukua udongo ambao ulikuja nao darasani. Unaweza kuwa udongo ambao huchimbwa na kuchanganywa na maji, au udongo ule unaotumiwa na watoto wadogo.)

Sema: Oneni udongo huu mikononi mwangu. Hufanyika mfano ule ambao njinaufinyanga. Unaweza kuwa mrefu kama nyoka au mfupi na mnono kama mkate. Naweza kuutengeneza uwe kama chungu, au niufunge kama kamba. Mimi mwenyewe huamua jinsi utakavyokuwa.

Nabii ambaye tunajifunza habari zake leo, alijifunza jambo muhimu alipomwona mfinyanzi akitengeneza chombo fulani. Kwanza hebu tuyaangalie maisha na ujumbe wa nabii

huyu. Halafu tutajifunza juu ya safari yake ya kwenda nyumbani kwa mfinyanzi.

Yeremia alianza kutoa unabii wakati wa utawala wa Mfalme Yosia. Baba yake Hilikia, alikuwa kuhani. Haikosi kwamba Yeremia aliweza kujifunza habari za Mungu akiwa nyumbani. Pengine alijifunza pia kutoka kwa babake habari za kutotii kwa watu wa Mungu.

Mchague mwanafunzi mmoja asome Yeremia 1:4-10.

Uliza: Je! Mungu alisema alimjua Yeremia lini? (Kifungu cha 5, Mungu alimchagua kabla ya kuumbwa tumboni mwa mama yake.)

Uliza: Je! Mungu alikuwa na mpango gani na Yeremia? (Kifungu cha 5, Mungu alimchagua kuwa nabii wa mataifa.)

Sema: Je! unashangazwa kwamba Mungu alikuwa na mpango na Yeremia wakati kama huu? (Wape muda wa kujibu). Sijui kama mnajua kwamba Mungu yu na mpango na kila mmoja wenu. Mungu amemwumba kila mtu kwa kusudi fulani na mpango maalum wa kutekeleza. Yeremia aliandika katika kitabu chake maneno haya, "Maana nayajua mawazo ninayo-wawazia ninyi, asema Bwana ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho." (Yeremia 29:11)

Uliza: Je! Yeremia aliitikiaje mwito wa Mungu? (Kifungu cha 6, Alitoa kisingizio juu ya umri wake na kutoweza kujua kusema.) Sema: Bwana alimwambia Yeremia asiseme kwamba yungali mtoto. Yeye angeenda na

afanye yote ambayo Bwana alimwambia afanye.

Uliza: Je! Mungu alimwahidi Yeremia nini? (Kifungu cha 8, Asiogope kwa sababu yeye yuko pamoja naye na atamwokoa.)

Uliza: Je! ni ukweli gani ambao tunaweza kujifunza kutoka kwa vifungu hivi? (Andika majibu yao ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Baadhi yao ni: (1) Mungu huwatumia watu wa umri wa wote kufanya kazi yake. (2) Hatupaswi kutoa visingizio wakati Mungu anapotutaka tumfanyie kazi. (3) Hatupaswi kuogopa iwapo tunatii maagizo ya Mungu.)

Eleza kwa kifupi hadithi ya Yeremia jinsi ilivyosimuliwa katika somo la wanafunzi.

Sema: Yeremia hakusaidia wala kuhimizwa na watu wake mwenyewe. Watu walimwelewa vibaya, waka-mlaumu, wakamtukana na waka-mfunga gerezani. Hali yeye alimtii Mungu hata ingawa haikuwa rahisi. Alikuwa nabii mwenye ujasiri.

Uliza: Je! unafikiri kwamba unaweza kuwa na ujasiri kama Yeremia? (Wape muda wa kujibu.)

Sema: Mungu alitaka kumfundisha Yeremia jambo fulani alipoenda nyumbani kwa mfinyanzi. Bila shaka Yeremia alikuwa amewahi kwenda huko, lakini Mungu alimtaka arudi huko tena.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yeremia 18:1-6.

Uliza: Je! Yeremia aliona nini alipoenda nyumbani kwa mfinyanzi? (Mfinyanzi alikuwa akitengeneza chombo fulani.)

Uliza: Je! mfinyanzi alifanya nini wakati chombo kile kilipoharibika? (Alianza tena kukitengeneza upya.)

Sema: Mungu alimfundisha Yeremia jambo fulani kutokana na kitendo hiki. Mungu aliwataka wale wanaomfuata kuwa watiifu jinsi udongo ulivyo mikononi mwa mfinyanzi. Lakini taifa la Yuda lingeamua cha kufanya kulingana na uhusiano wao na Mungu. Mungu angeendelea kuwaadhibu iwapo hawangetubu. Alikuwa kama mfinyanzi aliyetengeneza upya chombo kilichoharibika. Mungu aliwapenda watu wake, naye angeendelea kufanya kazi pamoja nao. Hangewaangamiza kwa sababu ya kutotii kwao. Lakini Mungu aliwataka waitikie mwito wa upendo wake kwa kuwa watiifu.

Sema: Tajeni baadhi ya njia ambazo tunapaswa kuwa kama udongo wa mfinyanzi. (1) Tunapaswa kumwacha Mungu (mfinyanzi) kutufanya tuwe jinsi atakavyo. (2) Tunapaswa kutubu tunapokosa na tumpe mfinyanzi nafasi ya kuweza kuturekebisha. (3) Tunapaswa kutambua kwamba Mungu anaweza kutufanya tuwe wa kutimika katika kazi yake, jinsi chombo kiwezavyo kuwa cha kutimika.)

Sema: Sasa semeni baadhi ya mambo tufanyayo ambayo yanaweza kutuzuia kutokuwa watiifu na wa kutimika. (Baadhi yake ni: (1) Tunataka kufanya mambo jinsi tutakavyo, wala sio vile Mungu atakavyo. (2) Tunataka kuwa kama rafiki zetu wala si kama vile Mungu ametupangia tuwe. (3) Hatumwamini Mungu pamoja na maisha yetu, lakini tunaamini vitu tuonavyo.)

Sema: Je! ungependa leo Mungu akufinyange na akutumia katika kusudi alilionalo kwako?

Andika ubaoni maneno ya wimbo usemao, "Mapenzi yako Yafanyike."

Mapenzi yako yafanyike
Wewe mfinyanzi, mimi towe,
Unifinyange upendavyo,
Mimi tayari, naja kwako.

Imbeni wimbo huu kimoyomoyo kama ombi lenu.

KAZI YA KUFANYA

Kuna maswali ambayo unayo yanayohusu Yeremia. Hebu jifanye kama unamwandikia barua. Katika mwisho wa barua hiyo, andika majibu ambayo unadhani Yeremia atasema.

Kwa rafiki Mpendwa, Yeremia,

Tafadhali, unaweza kujibu maswali yafuatayo:

1. Je! baba yako aliitwaje?
2. Je! ulikuwa ukiishi wapi?
3. Je! ni kisingizio gani ulichomtolea Mungu alipo-kwambia kwamba ana kazi ya kumfanyia?
4. Je! Mungu alikuahidije? Asante kwa kunisaidia ili nikufahamu vizuri.

Ni mimi

Rafiki yako

Tafuta majibu ya maswali haya kutoka kwa Maandiko ya Biblia na uyaandike.

1. (Yeremia 1:1): Hilkia, mmoja wa makuhani.

2. (Yeremia 1:1): Anathothi.

3. (Yeremia 1:6): Mimi ni mtoto tu.

4. (Yeremia 1:8): Nipo pamoja nawe na nikuokoe.

Mungu alisema na Yeremia na akamfundisha jambo muhimu akiwa nyumbani kwa mfinyanzi. Soma Yeremia 18:1-6 na ujibu maswali haya yahasuyo yale aliyoona.

1. Je! Yeremia aliona nini nyumbani kwa mfinyanzi? (Kifungu cha 3) Alimkuta akiwa anafanya kazi yake kwa gurudumu.
2. Je! ni nini kilichofanyika kwa chombo ambacho mfinyanzi alikuwa akitengeneza? (Kifungu cha 4) Kiliharibika.
3. Je! mfinyanzi alikifanyaje kile chombo kilichoharibika? (Kifungu cha 4) Alikifanya tena kuwa chombo kingine.
4. Je! Yeremia alijifunza nini kutokana na jambo hili? (Kifungu cha 6) Kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo tulivyo katika mkono wa Mungu.

Mungu ni mfinyanzi wa maisha yetu. Anatutaka tumwitikie jinsi udongo ulivyo mikononi mwa mfinyanzi.

Mungu ni pendo. Yeye ni mfinyanzi mvumilivu ambaye hutusamehe na kutufanya upya ili tuwe kama Yesu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Angalieni, kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, Ee nyumba ya Israeli" (Yeremia 18:6b).

SWALI LA MALAKI: "JE! MWANADAMU ATAMWIBIA MUNGU?"

MASOMO YA BIBLIA: Malaki 3:6-12
KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wanafunzi wanajua jinsi pesa zitolewazo kanisani hutumiwa? Je! wanaelewa maana ya kutoa zaka na wajibu wa Mkristo wa kutoa? Somo hili litawasaidia kuelewa umuhimu wa kutoa zaka na sadaka kanisani.

Ni vigumu kufundisha ukweli ambao haujawahi kuukabili wewe mwenyewe. Huu unaweza kuwa wakati wako wa kujitoa, iwapo hujawahi kuona baraka ambazo mtoaji zaka hupata. Neno la Mungu ni lako, na ahadi zake za baraka ni za kweli.

1. Soma somo lililoko katika kitabu cha wanafunzi. Mwombe Mungu akusaidie ili uweze kumchagua mwanafunzi anayefaa ili asome sehemu ya Chege wakati wa kujifunza somo hili.

2. Soma somo lililoko katika kitabu cha mwalimu. Rudia tena kusoma kuhusu miaka ya manabii ambayo imeandikwa katika mfululizo wa somo hili. Uwe tayari kuandika ubaoni, majina ya manabii na karne ambazo walikuwa wakitoa unabii wao.

3. Mwalike shemasi au mchungaji wakati wa mwisho wa somo hili ili aje kueleza kuhusu vile sadaka hutumika katika kanisa.

4. Uwe na sarafu kumi za senti kumi ili uonyeshe maana ya kutoa "zaka".

Malaki: Ni machache tu yanayojulikana kuhusu Malaki. Jina lake linamaanisha, "mjumbe wangu," naye alitoa unabii mnamo mwisho wa karne ya sita hadi mwanzo wa karne ya tano. Watu wa Israeli walikuwa wamesharudi nyumbani kwao na hekalu lilikuwa limejengwa tena upya. Hata hivyo, watu wenyewe hawakuwa na furaha wala hawakumwabudu Mungu kwa moyo wa kweli. Kulikuwepo na ukame, njaa na mimea iliharibika sana. Watu hao hawakujishughulisha wala kumwendea Mungu. Walishuku mapenzi ya Mungu kwao na kujiuliza juu ya faida ya kumfuata.

Malaki aliandika kama kwamba Mungu alikuwa akiongea na watu wake. Kuna maswali saba ambayo yameulizwa na kujibiwa, yanayohusu dhambi za Israeli.

SOMA MAANDIKO

Kitabu cha Malaki kina sura tatu tu. Kwa hivyo, utapaswa kukisoma tena na tena ili ukielewe vizuri.

Malaki, kama vile manabii wengine, aliwaonya Wayahudi juu ya dhambi zao kwa Mungu. Baadhi ya dhambi ambazo Malaki alizungumzia ni:

1. Kuuliza juu ya uthibitisho wa mapenzi ya Mungu. (1:2)
2. Kutoheshimu jina la Mungu. (1:6)
3. Kutoa chakula kilichotiwa unajisi katika madhahabu. (1:7)

4. Kuvunja ahadi za ndoa. (2:14)
5. Kutoleta zaka katika ghala la Mungu. (3:8)

6. Kuongea kwa lugha ya kumkosea Mungu. (3:13-14)

Nabii huyu alikuwa na jawabu - Jibu kutoka kwa Mungu. Mungu angemtuma mjumbe wake ambaye angemtarishia Masihi njia. (3:1-4)

Somo la leo litatoka katika sura ya 3:6-12.

Kifungu cha 6: Mungu habadiliki. Habadiliki kwa mapenzi yake wala habadiliki kwa kutaka utifu.

Kifungu cha 7: Mungu aliwaambia Wayahudi wamrudie. Mungu aliwapatia nafasi nyingine ya kumrudia kwa sababu ya huruma zake.

Kifungu cha 8: Wakauliza, "Je! mwanadamu atamwibia Mungu?" Bwana aliwajibu swali hili kwa kuwaonyesha vile walivyokuwa wamemwibia. Walikuwa wamemwibia Mungu sio kwa vile walivyokuwa wamechukua, bali kwa vile ambavyo walikuwa wamekataa kutoa. Watu hao hawakuwa wameleta zaka na sadaka zao katika nyumba ya Bwana.

Kifungu cha 9: Taifa lote lilihusika katika dhambi ya kumwibia Mungu. Kwa hivyo wote wangukuwa chini ya hukumu ya Mungu.

Kifungu cha 10: Mungu aliwaamuru walete zaka kamili ghalani. Halafu akawaahidi baraka zake ambazo wangepata iwapo wangemtii.

Kifungu cha 11 na 12: Mungu anataja vile atakavyowabariki: atazuia wadudu wasiharibu mimea yao, mizabibu itatoa

matunda na jirani zao wataona maendeleo yao na watawaita waliobarikiwa.

Kusudi la somo hili ni *kuwasaidia wanafunzi waelewe maana na umuhimu wa kutoa zaka na sadaka kanisani, na kuwahimiza kujitoa kuwa watoaji.*

KULIFUNDISHA SOMO

Andika ubaoni majina ya manabii ambao umejifunza habari zao katika masomo kumi yaliyopita. Andika pia karne ambayo walitoa unabii wao kando ya majina yao. Orodha hii ifuatayo itausaidia:

ELIJAH	-----9
AMOSI	-----8
HOSEA	-----8
ISAYA	-----8
MIKA	-----8
SEFANIA	-----7
NAHUMU	-----7
HABAKUKI	-----7
YEREMIA	-----7

Sema: Wakati hasa wa huduma ya nabii ambaye tunajifunza habari zake leo haujulikani. Inafikiriwa kwamba Malaki alitoa unabii wake mnamo mwisho wa karne ya sita hadi mwanzoni mwa karne ya tano.

Ni habari chache tu zinazojulikana juu ya Malaki. Yeye pia kama manabii wengine, aliwaonya watu wa Israeli juu ya dhambi zao.

Uliza: Juma lililopita tulijifunza kuhusu Yeremia. Je! mnaweza kukumbuka kilichofanyika kwa Waisraeli wakati huo? (Walikuwa

wameshikwa mateka na jeshi la adui zao na kupelekwa Babeli.)

Sema: Kwa sasa, walikuwa wamerudi nyumbani kwao na kuishi huko kwa muda wa miaka mia moja. Walikuwa na shukurani kwa huruma za Mungu hapo mwanzoni waliporudi kwao. Halafu walianza kubadilika na kutomjali Mungu. (Andika ubaoni dhambi walizotenda.)

Baadhi ya dhambi ambazo Malaki aliwaonya Wayahudi ni:

- (1) kutoitikia mapenzi ya Mungu.
- (2) kutoheshimu jina la Mungu.
- (3) kumwibia Mungu zaka na sadaka.
- (4) kuwapatia talaka wake zao, na
- (5) kutoa dhabihu zilizotiwa najisi.

Leo tunataka tufikirie juu ya maana ya mojawapo ya mafundisho ya Malaki: kumwibia Mungu zaka na sadaka. Nimemwuliza (sema jina la mwanafunzi) anisaidie kueleza jambo hili. (Mwambie mwanafunzi huyo akae mbele ya darasa na ajaribu kutafuta kitabu cha Malaki katika Biblia. Endelea na mchezo huu.)

Uliza: (Andika neno “zaka” ubaoni.) Ni nani awezaye kuniambia maana ya “zaka” baada ya kusikiliza mchezo huu. (Rudia jibu lao ili wote wasikie)

Sema: Neno “zaka” linamaanisha “sehemu moja ya kumi.” (Waonyeshe sarafu kumi za senti kumi ambayo umeleta na uwaeleze kuwa senti moja ni sehemu ya kumi ya senti yote kumi.)

Uliza: Kama mtu atapata shilingi 100, je! zaka yake itakuwa kiasi gani? (Shilingi 10 kwa mia au sehemu moja ya kumi ya pesa hizo.)

Uliza: Je! ni nani anajua vile pesa zitolewazo kanisani hutumia? (Wape muda wa kujibu. Rudia majibu yaliyo sawa ili watu waweze kusikia.)

Sema: Leo nilimwuliza (shemasi au mchungaji au mweka hazina wa kanisa) kutuambia vile ambavyo pesa zinazotolewa hutumika kanisani. (Ikiwa watu hawa hawapo, basi utapaswa kueleza jinsi sadaka huhesabiwa na kuwekwa, na kutumiwa)

Uliza: Je! mnaona umuhimu ulipo kwa kila mshiriki wa kanisa kuweza kutoa ili kulipia matumizi ya kanisa?

Sema: Mungu hutuahidi baraka zake ikiwa tutakuwa waaminifu kwa kumtolea zaka na sadaka.

Wahimize wanafunzi wako wamalizie sehemu ya KAZI YA KUFANYA iwapo hawajaikamilisha.

KAZI YA KUFANYA

1. Soma Malaki 3:6-9 na uweke alama hii (✓) kando ya sentensi iliyo kweli.

✓ Bwana habadiliki.

✓ Wayahudi walikuwa waaminifu katika kutii amri za Mungu.

— Wayahudi walikuwa wamekosa kumtii Mungu kwa muda mrefu.

— Mungu hangewaadhibu kamwe Wayahudi.

✓ Taifa lote lilikataa kumtii Mungu.

2. Soma Malaki 3:8-12 na ujaze nafasi zilizoachwa.

Mungu alisema kwamba watu walikuwa wamemwibia zaka na sadaka. Jambo hili lingelifanya taifa lote lipate laana, Mungu angemwagia baraka iwapo watu hao wangetubu na kuleta zaka zao kamili ghalani. Mungu naye hangewaacha wadudu waharibu mazao yao. Mataifa mengine yangeweza kuona jinsi wanavyo-pendeza na kuwaita wenye heri.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi, mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la” (Malaki 3:10).

Kifungu chetu cha kukumbuka ni amri iliyo na ahadi. Iwapo watu watatoa zaka na sadaka zao zote, basi kutakuwa na mali ya kutosha ya kusaidia kazi ya Mungu. Nao watu wa Mungu watabarikiwa sana.

3. Andika katika nafasi ifuatayo amri na ahadi iliyotolewa katika kifungu cha 10.

Amri ya Mungu (kifungu cha 10a)
Leteni zaka kamili ghalani.

Ahadi ya Mungu (kifungu cha 10b)
Nitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka.

Andika kifungu cha kukumbuka ubaoni au kwenye karatasi kubwa. Kifungu hiki ni kirefu sana kuliko vile vingine ambavyo wanafunzi wameshajifunza, kwa hivyo watataka wasaidiwe kuweza kukariri. Kifundishe kwa kutumia vitendo vifuatavyo.

LETENI ZAKA KAMILI GHALANI
- (Jifanye kama unaweka sadaka zako katika chombo cha sadaka.)

ILI KIWEMO CHAKULA KATIKA NYUMBA YANGU - (Jifanye kuwa unakula chakula.)

MKANIJARIBU KWA NJIA HIYO, ASEMA BWANA WA MAJESHI - (Nyoosha mikono yako ukiielekeza mbinguni.)

MJUE KAMA SITAWAFUNGULIA MADIRISHA YA MBINGUNI - (Jifanye kuwa unafungua dirisha.)

NA KUWAMWAGIENI BARAKA, HATA ISIWEPO NAFASI YA KUTOSHA, AU LA - (Telemsha mikono yako chini ukiielekeza sakafuni.)

WAKATI WA MWISHO

Sema: Katika sehemu ya mwisho wa somo lenu, kuna “ahadi yako ya kutoa zaka.” (Hebu fungua mahali hapo katika somo la wanafunzi.)

Tafadhali ombeni sasa jinsi mtakavyo amua kumtolea Mungu zaka ya vitu vyote ambavyo amwezesha kupata na vile ambavyo mtapata baadaye. Huu unaweza kuwa uamuzi wa maana sana kwako. Mungu anakutaka uwe mwaminifu kwake hata ingawa kwa sasa hupati pesa nyingi. Kumbuka kwamba, kila kitu ni mali ya Mungu. Unatoa tu sehemu ndogo ya mali yake ili kuwezesha kazi yake ifanyike kanisani.

Omba, au umwambie mwanafunzi mmoja aombe kwamba washiriki hawa wasiwe na hatia ya kumwibia Mungu au kukosa kupokea baraka zake alizotuahidi.

SURA YA KUMI NA MBILI

MUNGU ANAWAPENDA WATU WOTE

MASOMO YA BIBLIA: Yona 1:1-3;
3:1-5; 4:1-6

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Je! wana shida ya kutoweza kuwatendea washiriki wengine kwa njia iliyo sawa? Je! Washiriki wa darasa lako wanaotoka katika nchi ya kigeni au wa kabila fulani wanaheshimiwa?

Karibu kila mmoja wetu ana ubaguzi maishani mwake. Kuwa na ubaguzi ni kuwazia wenzako au kuwachukia. Maoni na mawazo ya ubaguzi wa watu wengi hukua wakati wanapokuwa wangali wadogo. Hujifikiria kuwa na tabia za watu wazima za kusema kwa ukali kwa wenzao.

Mawazo haya ya ubaguzi yaweza kuwazuia vijana kwa kutotimiza kusudi la Mungu kwao. Mawazo mabaya huleta ushirika mbovu ambao husababisha matendo mabaya. Vijana wanapaswa kutambua kwamba Mungu anaweza kuwasaidia kushinda nia zao mbaya.

Somo hili lihusulo Yona litalisaidia darasa lako kuona jinsi Mungu awezavyo kutimiza kusudi lake bila kujali makosa au udhaifu wa mwanadamu. Watajifunza kwamba Mungu hutumia watu kwa kutimiza mapenzi yake.

Mwombe Roho Mtakatifu awe mwalimu wako unapojifunza somo hili. Mwombe Mungu akusamehe iwapo kuna watu wa kabila au nchi fulani ambao unapata shida kuwapenda au

kuwasikiliza. Hutafundisha somo hili vizuri iwapo unalifikiria kabila au taifa lako kuwa bora kuliko mengine yote.

Yona alikuwa nabii wa Agano la Kale aliyekuwa na mawazo ya ubaguzi maishani mwake. Mungu alimwita ili akawahubirie watu wa Ninawi lakini hakutaka kwenda. Yona aliwachukia watu walioishi huko, na hakutaka kuwaona kutoka katika uovu wao.

Yona alikuwa Myahudi, mtoto wa Amitai, nalo jina lake lilimaanisha "huwa". Tunaambiwa katika 2 Wafalme 14:25 kwamba alikuwa akiishi Gatheferi, sehemu ya kaskazini mwa Nazareti.

Yona yuko tofauti sana na manabii wengine ambao tumejifunza habari zao katika mfululizo wa masomo haya. Kitabu cha Yona kinatuelezea nabii huyu badala ya kutuambia habari za mahubiri yake. Zaidi ya nusu ya kitabu hiki kinatuelezea jinsi Mungu alivyojaribu kumwondolea Yona majivuno yake. Yona alipatwa na jambo la ajabu kabla ya kukubali kuitikia mwito wa Mungu.

SOMA MAANDIKO

Madokezo yafuatayo yatakusaidia unapojifunza kitabu hiki cha Yona.

Sura ya 1: Nabii asiye mtiifu. Mungu anamwita Yona ili aende Ninawi. Badala ya kwenda huko anaenda Tarshishi. Kunatokea dhoruba kali baharini na hatimaye anamezwa na samaki mkubwa.

Sura ya 2: Nabii mwenye kutubu. Yona anatubu akiwa tumboni mwa samaki. Hatimaye anaomba na kuokolewa.

Sura ya 3: Nabii mtiifu. Mungu anamwita tena Yona ili aende Ninawi. Wakati huu anamtii Mungu. Anahubiri, nao watu wanatubu.

Sura ya 4: Nabii aliyeudhika. Ninawi inaokolewa lakini Yona anakasirika sana. Anakaa chini ya kivuli cha mti ambao hatimaye unakauka. Mungu anatumia mfano huu kwa kueleza juu ya Ninawi, hasa kuhusu huruma na msamaha wake.

Masomo yetu ya Biblia ya leo yatatoka katika sura tatu tofauti.

Yona 1:1-3: Nabii huyu alikuwa akifurahia huduma yake nzuri aliposikia mwito wa Mungu. Mungu alimtaka Yona kwenda Ninawi na kuhubiri kwamba mji huo ungepatwa na hukumu yake. (1:1-2) Lakini, badala ya yeye kumtii Mungu, alienda katika bandari ya Yafa na akapanda katika merikebu iliyokuwa inaelekea Tarshishi. Alienda sehemu nyingine badala ya kwenda Ninawi. Alijaribu kumkimbia Mungu, lakini alitambua kwamba hangeweza kutoroka Mungu.

Yona 3:1-5: Yona alitii alipoitwa mara ya pili. Alienda Ninawi na akahubiri ujumbe wa Mungu uhusuo kuangamizwa kwa watu wote.

Ninawi ulikuwa mji mkubwa sana. Ilimchukua mtu siku tatu kuweza kupita mji wote. Baadhi ya wanafunzi waliosoma Biblia wanasema kwamba mji huu ulikuwa na upana kilomita mia. Watu walimsikiliza Yona akihubiri nao wakatubu dhambi zao. Mungu alikuwa

ametayarisha mioyo ya watu hao kusikia, nao waliposikia walianini.

Yona 4:1-6: Ninawi ulikuwa mji mkuu wa taifa la Ashuru. Wayahudi walikuwa wakiteswa sana na Waashuru, na Yona aliwachukia sana watu hawa. Lakini sasa, Yona alikasirika sana wakati maelfu ya Waashuru walipoitikia mahubiri yake. Alikuwa amemtii Mungu lakini mawazo yake hayakuwa yamebadilika. Alitaka afe badala ya kumwona Mungu akiwahurumia maadui wa Israeli.

Yona alikuwa amekasirika sana alipotoka mjini humo. Alijijengea kibanda, akakaa chini ya kivuli chake na akangojea kuona mji ule utakuaje. Hatimaye aliutambua mmea ulikuwa unakua haraka sana. Yona alifurahi sana kukaa chini ya kivuli chake. Muda si muda mmea ule ulianza kunyauka na kukauka.

Mungu alimkemea Yona kwa sababu ya mawazo yake. Yeye aliifikiria starehe yake kuwa ya muhimu sana kuliko watu wa mji ule waliokuwa wakifa katika dhambi.

Kitabu hiki hakituambii juu ya mwisho wa hadithi hii, kwa hivyo kila mmoja anaweza kuikamilisha hadithi hii yeye mwenyewe akijiweka katika nafasi ya Yona. Je! Utaonyesha upendo wa Mungu kwa watu wachache au kwa kabila moja tu? Je! utawashughulikia watu wote kwa kutojali rangi, kabila au hali waliyonayo? Je! utafurahi wakati uonapo watu wakiitikia ujumbe wa Mungu wa upendo? Je! utausikiliza ujumbe wa Mungu vyema kuliko Yona?

Kusudi la somo hili nikuwahimiza wanafunzi kuwaonyesha watu wote upendo bila ubaguzi.

KULIFUNDISHA SOMO

Waambie wanafunzi kadhaa waige mchezo huu ulioko mwanzoni mwa somo lao. Darasa lote laweza kushiriki. Wanafunzi wachache wanaweza kutoka nje na kuingia tena darasani na kujifanya kuwa ni wageni. Wanaweza kuvaa mavazi tofauti ikiwa watataka hivyo. Waambie waonyeshe sura ya mshangao. Washiriki wa darasa wataipaswa kuwaangalia na kusemezana kati yao kuhusu wageni. Mwanafunzi mmoja atapaswa kuwa mhubiri wa ujumbe wa asubuhi. Mgeni Mgeni mmoja atajitokeza mbele na kuanza kusema na mchungaji.

Mchungaji naye ataliambia kanisa kwamba mgeni yule amempokea Kristo kama Mwokozi wake.

Uliza: Je! kunaye mmoja kati yenu ambaye amewahi kujisikia kama mgeni huyu? (Wangoje waeleze vile walivyojisikia)

Uliza: Je! Tunaweza kufanyaje ili tuepuke tatizo hili kanisani au darasani mwetu. (Waruhusu watoe maoni yao ambayo yatasaidia wakati wageni wafikapo.)

Sema: Hadithi yetu ya leo inamhusu nabii aitwaye Yona. Alikuwa Myahudi naye alijivuna sana. Hata alifikiria kwamba Mungu anapaswa kuwadhibu madui wa Israeli, badala ya kuwaokoa. Alikuwa na ubaguzi kwa watu wengine ambao hawakuwa Wayahudi.

Uliza: Ni nani anayejua maana ya ubaguzi? (Andika neno hili ubaoni, na uandike pia majibu ya wanafunzi hao. Majibu yao yanapaswa kuwa na maana

hii: Mawazo au nia mbaya kwa watu wengine au kabila fulani.)

Sema: Yona aliwachukia sana watu wa Ninawi. Wao walikuwa maadui wa Wayahudi na pia walikuwa watu wa Mataifa.

Simulia hadithi ya somo hili, au mwambie mwanafunzi mmoja akusaidie kuisimulia. Andika vichwa vifuatavyo ubaoni kama dokezo:

1. Kuitwa kwa Yona
2. Kutotii kwa Yona
3. Kutubu kwa Yona
4. Ujumbe wa Yona
5. Kukasirika kwa Yona
6. Kukemewa kwa Yona na Mungu.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Yona 4:1-4.

Uliza: Je! kwa nini Yona alikasirika? (Hakumtaka Mungu awahurumie watu ambao walikuwa maadui wa Israeli.)

Uliza: Je! Yona alimwomba Mungu nini? (Alimwomba amwache afe.)

Uliza: Je! Mungu aliitikiaje katika kifungu cha 4? (Alimwuliza Yona iwapo alifanya vizuri alipokasirika)

Mwambie mwanafunzi mwingine asome 4:5-6.

Uliza: Je! Yona alifanyaje wakati mmea ule ulipokua na kumfanyia kivuli? (Alifurahi sana.)

Sema: Mtango ule haukudumu sana. Mungu alitayarisha buu aliyeula mtango huo na ukakauka.

Soma katika Biblia yako Yona 4:10-11.

Uliza: Je! nia ya Yona ilipinganaje na ule mtango ikilinganishwa na nia yake kwa watu wa Ninawi? (Alijishughulisha sana na kukauka kwa mtango ule kuliko alivyofikiria juu ya kufa kwa watu bila kumjua Mungu.)

Uliza: Je! Mungu alitaka amfundishe Yona nini katika vifungu hivi viwili? (Mungu anawajali watu wote. Upendo na wokovu wake ni kwa watu na makabila yote.)

Uliza: Je! kunao watu ambao huwapendi? Au kabila fulani? Au watu wa rangi fulani?

Sema: Kila mmoja wetu ni wa muhimu kwa Mungu. Humtunza kila mmoja kwa njia maalum.

Uliza: Je! tunapaswa kuwa na mawazo yapi baada ya kujua kwamba Mungu anawapenda watu wote? (Tunapaswa kuanza kuwapenda watu wa rangi au kabila lo lote na upendo kama ule wa Kristo.)

Waambie wanafunzi wafungue sehemu ya KAZI YA KUFANYA ya somo lao.

KAZI YA KUFANYA

Soma kila sentensi ifuatayo, na ujaze kwa neno lililosahihi katika nafasi iliyoachwa. Maneno yenyewe yameandikwa chini ya sentensi hizi.

1. Mungu alimwambia Yona aende Ninawi.
2. Yona alienda katika bandari ya Yafa na akapata merikabu ikiwa inaenda Tarshishi.
3. Alipokuwa kwenye merikabu ile kulitokea dhoruba kuu.

4. Mabaharia walimtupa Yona baharini. Mungu alikuwa amemtararisha samaki mkubwa ili ammeze Yona.

5. Yona alikuwa ndani ya tumbo la samaki kwa muda wa siku tatu mchana na usiku.

6. Yona alitubu wakati alipokuwa tumboni mwa samaki.

7. Yona alihubiri ujumbe ambao Mungu alikuwa amempa, alipofika Ninawi. Aliwaonya kwamba Mungu angeuangamiza mji wa Ninawi baada ya siku arobaini.

8. Watu wa Ninawi walitubu waliposikia ujumbe wa Mungu.

9. Mungu hakuuangamiza mji huo kwa sababu ya kutubu kwao.

Maneno: Ninawi, siku tatu, walitubu, Tarshishi, arobaini, dhoruba, alitubu, samaki, hakuuangamiza.

Soma Yona 4:1-4, na uchore mvingo kwenye jibu lililosawa la maswali yafuatao:

1. Je! kwa nini Yona alikasirika?

- a. Yule samaki mkuu alitoweka.
- b. Mungu aMkuwa amem-danganya.

c. Watu wa Ninawi walitubu.

2. Je! Yona alimwambiaje Mungu?

a. Umebadili nia yako.

b. Wewe ni Mungu mwenye mapenzi na rehema.

c. Unawapenda tu Waisraeli.

3. Je! Mungu alimjibuje Yona?

a. Waweza kufa ukitaka.

b. Mimi nakupenda. Tafadhali usikasirike.

c. Je! unatenda vema kukasirika?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Kwa maana siionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia” (Warumi 1:16).

Uliza: Je! kifungu hiki kina-tufundisha kwamba ni nani ambaye atapokea wokovu? (Kila mmoja)

Uliza: Je! kuna watu ambao huwapendi? Je! kwa nini usimwombe Mungu sasa akuondolee ubaguzi wako?

WAKATI WA MWISHO

Uliza: Je! ulitoaje orodha ya watu walioandikwa hapo chini?

Kuna orodha ya watu tofauti hapo chini. Wapange kuanzia mtu wa kwanza hadi wa kumi. Mfanye mtu wa kwanza (1) awe yule ambaye unaweza kumpenda kwa urahisi. Na yule wa 10 awe mtu ambaye unapata shida la kumpenda.

___Mtoto wa mtawala
___Mwana michezo hodari
___Askari au Polisi

Uliza: Je! unafikiri kwamba Mungu anawapenda watu fulani kuliko wengine? Weka alama hii (✓) kwenye jibu lako. () Ndiyo () La.

Yona alijifunza kwamba Mungu anawapenda watu wote. Jaribu wiki hii kumwambia mtu wa kabila lingine juu ya upendo wa Yesu Kristo. Mwambie kwamba Mungu anawapenda na hata wewe unampenda pia.

Ombeni pamoja. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi hao ili waweze kujifunza ukweli wa somo hili. Omba kwamba Mungu atawapa moyo wa kuwapenda watu wote.

___Binamu yako (mtoto wa ndugu ya baba au mama.)
___Mtu wa kabila lingine
___Mtu wa nchi nyingine ya Afrika
___Mtu wa rangi tofauti na yako
___Kilema
___Mfungwa
___Mzee

KUWA NA UJASIRI WAKATI WA HATARI

MASOMO YA BIBLIA: Danieli 6:7; 10-11; 16-23

KUJIANDAA KUFUNDISHA

Wafikirie wanafunzi wa darasa lako. Unapaswa kuwa na ujasiri wa kuwa na msimamo hata ikiwa si jambo la kuwapendeza watu. Danieli alifanya mambo yaliyomema hata wakati alipokuwa katika hatari.

Danieli alikuwa na uhusiano mwema na Mungu kupitia kwa maombi yake ya kila siku. Vijana wanapaswa kujua pia umuhimu wa maombi maishani mwao. Mtu hujua jinsi ya kumtegemea Bwana wakati wa shida anapokuwa na wakati wa maombi pamoja na Bwana kila siku.

Somo hili lihusulo Danieli litasaidia darasa lako kuona jinsi Danieli alivyobakia mwaminifu kwa Bwana wakati wa shida. Hakuacha mazoea yake ya kumwomba Bwana ili kuzuia kutopata madhara.

Vijana wengi hawataki kuwa tofauti. Hutaka kusema na kufanya mambo ambayo yatawafanya wakubaliwe mbele za rafiki zao. Ni vigumu kusimama peke yako na kukubali kudhihakiwa kwa sababu ya kuwa "mwamini wa dini". Danieli alikuwa kijana ambaye alikuwa tayari kuonekana tofauti.

Waombee wanafunzi wako ili wawe na mazoea ambayo yatawasaidia kusimama imara wakati wa shida. Jiombee wewe unapotayarisha somo hili. Fikiria jinsi uwezavyo kuwahimiza

washiriki wa darasa lako ili wawe kama Danieli.

Hakuna habari nyingine inayojulikana pasipo kitabu hiki, ambayo inamtaja Danieli kuwa mhusika mkuu. Jina lake linamaanisha kwamba, "Mungu ndiye hakimu." Wanahistoria wanaamini kwamba Danieli alizaliwa Yerusalemu, lakini hawajahakikisha jambo hili.

Nebukadneza aliwapeleka vijana hodari wa Israeli kule Babeli aliporudi huko kutoka Yerusalemu mnamo mwaka wa 605 B.C. Danieli alikuwa baadhi ya vijana hawa. Sura ya 1:3-4 inasema kwamba mateka hawa walikuwa watoto wenye tabia nzuri, wasio na kasoro, wenye umbo la kupendeza, wenye hekima, na maarifa na wawezao kutumika katika makao ya mfalme. Mfalme alimpenda sana Danieli pamoja na rafiki zake watatu. Wote watatu walipewa madaraka ya uongozi. Danieli alitumika kama liwali mkuu kwa miaka sabini akiwa Babeli.

Haikosi kwamba kulikuwepo na majaribu mengi kwa kijana kama huyu ambaye alikuwa mbali na nyumbani kwao, jamaa na marafiki. Ingekuwa rahisi kwake kukubali desturi na tabia za nchi ya wasiowaamini ambako alikuwa akiishi. Lakini Danieli alitwa na Mungu kuwa tofauti.

SOMA MAANDIKO

Si rahisi kujifunza kitabu chote cha Danieli katika somo moja fupi. Kwa hivyo tutahusika tu na vifungu vichache

kutoka katika sura ya kwanza na vile vinavyolingana navyo katika sura ya sita.

Danieli 1:8-12. Ilikuwa ni desturi ya wakati wa Danieli kwa watawala kuchagua vijana wa kushika mateka na kuwafundisha jinsi ya kuwa watumishi waaminifu. Danieli na rafiki zake watatu walichaguliwa kwa kusudi hili na walienda kufundishwa kwa muda wa miaka mitatu. Baadaye, walipelekwa mbele ya mfalme.

Vijana hawa walichukuliwa kwa hali ya juu. Mfalme alisema kwamba wapewe chakula na divai ambayo yeye hutumia. Chakula cha mfalme kilikuwa bora na kikawa hata na divai ambayo haikuwa nzuri kwa afya ya mwili. Vijana hawa walikataa chakula walichopewa. Inaaminika kwamba chakula hiki hakikupikwa kulingana na imani ya Kiyahudi. Pengine kulikuwa na nyama na divai iliyotolewa kama dhabihu kwa sanamu.

Majaribio yalifanywa. Danieli na rafiki zake walipewa mboga na maji, na wale vijana wengine walipewa chakula cha mfalme. Wote walienda kukaguliwa baada ya siku kumi. Danieli na rafiki zake walipatikana wakiwa wazuri zaidi na wamenenepa (Kifungu cha 15). Walipewa vyeo vikubwa katika ufalme ulio kuu sana katika ulimwengu wa historia kwa sababu ya kujitawala kwao.

Danieli 6:7. Mfalme Dario alibadili mtindo uliotumiwa kutawala nchi yake alipofanywa mfalme. Alichagua maliwali (Governors) wa kusimamia sehemu 120 za nchi hiyo. Wasimamizi watatu, walioitwa raisi, walichaguliwa ili kuwasimamia maliwali hawa.

Danieli alipewa uraisi mara ya kwanza, halafu baadaye akapandishwa cheo. Alifanywa kuwa msimamizi wa ufalme wote.

Inaaminika kwamba kulikuwa na wivu kutoka kwa wale waliokuwa na vyeo vya chini. Hii inaweza kuwa ni kweli kwa sababu Danieli alikuwa Myahudi na mgeni kule Babeli. Maadui hawa walimfanyia Danieli njama ili aachishwe kazi hiyo yake.

Danieli 6:10-11. Maadui wa Danieli walijua kwamba alikuwa na mtindo wa kuomba mara tatu kwa siku. Hawakuweza kupata kosa katika kazi ya Danieli wala maishani mwake, kwa hivyo walishtaki ibada alizomfanyia Mungu.

Viongozi hawa wenye wivu walimwambia mfalme atie sahihi kwenye amri iliyosema kwamba mtu ye yote atakayemwomba Mungu mwingine isipokuwa mfalme kwa muda wa siku thelathini, atatupwa kwenye tundu la simba. Mfalme huyu mpya alitaka utiifu, kwa hivyo alikubaliana na sheria hii.

Watu hawa walienda kumwambia mfalme walipomwona Danieli akiendelea kuomba kama kawaida. Amri ya Wamedi na Waajemi ilikuwa imepitishwa nayo haingebadilishwa kamwe. Kwa hivyo, mfalme aliamuru kwamba Danieli atupwe kwenye tundu la simba.

Mfalme alionyesha heshima yake kwa Mungu wa Danieli, lakini hangeweza kumwokoia.

Danieli 6:16-23. Haikosi washtaki wa Danieli walidhania kwamba walikuwa

wamemwua adui yao kwa kutumia sheria. Danieli alitupwa katika tundu lile la simba, nao likafunikwa na jiwe kubwa, na mfalme akapiga mhuri wake juu yake.

Mfalme alirudi kwake ili kulala. Alikataa kula wala kuchezeva vinanda. Usiku huo hakuweza kulala.

Ilipokuwa ingali asubuhi na mapema, mfalme huyo aliamka na kwenda kwa tundu la simba. Alimwita Danieli. Halafu akamwuliza iwapo Mungu wake aliyemhudumia amemwokoa.

Danieli alimsalimia mfalme kwa salamu za heshima na akamwonyesha hitaji lake la kutaka aishi milele. Hatimaye alimwambia mfalme kwamba Mungu alimtuma malaika wake naye akayafumba makanwa ya simba wala hawakumdhuru. Danieli alimwambia kwamba Mungu alikuwa amemlinda kwa sababu hakuwa amekosa. Mwishowe Danieli alitoa heshima zake kwa mfalme.

Mfalme alisema kwamba watu wote waabudu na kumtumikia Mungu wa Danieli. Watu wale waliomshtaki Danieli walitupwa katika tundu la simba pamoja na jamaa zao.

Danieli alitumika chini ya wafalme watatu tofauti, naye alikuwa mtumishi mwema. Wakati huo pia, alikuwa mwaminifu kwa Mungu na hakubadili imani yake. Mungu alimtuza, na siku hizi Danieli anakumbuka kama nabii aliyemwamini Mungu kwa haki bila kutojali shida alizopata.

Kusudi la somo hili ni *kuwaongoza wanafunzi kuweza kuamini kwamba*

Mungu atawasaidia hata wakati wa shida.

KULIFUNDISHA SOMO

Sema: Mama mmoja aliamshwa akiwa amelala usiku alipoona mwangaza uliofuatiwa na ngurumo ya radi. Aliamka na akaenda kitandani pa mwanawe mdogo. Msichana huyo wake mdogo alikuwa ameogopeshwa sana na ngurumo hizo, kwa hivyo mamake alimwendea haraka sana.

Mtoto huyo alikuwa karibu kuondoka kitanda chake hali yu karibu kuanza kulia. Alipomwona mamake, alimnyoshea mikono yake. Mama huyu alimkumbatia mwanawe kwa muda mfupi, naye akashikwa na usingizi tena.

Uliza: Je! Umewahi kuogopa? (Wape muda wa kujibu.)

Uliza: Je! Unajua kwamba Mungu huonyesha upendo wake kwako kwa kukupa ujasiri wakati upatapwo na shida? Hadithi yetu ihusuyo Danieli itakusaidia kujua jinsi ya kumwamini Mungu hata wakati wa shida.

Tumia kitabu cha wanafunzi kama mwongozo, na usimulie hadithi ya Danieli na rafiki zake, jinsi walivyoshikwa na kupelekwa Babeli. Halafu waambie jinsi walivyokataa kunywa na kula vyakula ambavyo havikuwa bora kwao.

Sema: Matangazo ya Redio na Televisieni huwahimiza mnywe na mle chakula ambavyo havifai kwa afya zenu.

Uliza: Je! umeshawahi kushawishika kutaka kununua kinywaji au chakula ambacho umeona au kusikia kikitangazwa?

Sema: Ni juu ya mtu binafsi kuamua kula vyakula ambavyo havifai kwa afya yake. Lakini jambo hili huleta tuzo kubwa jinsi tuonavyo katika maisha ya Danieli. Alikuwa amechaguliwa kuwa mmojawapo wa watawala wa serikali. Hili lilikuwa jambo zuri kwa sababu alikuwa mgeni, mtumwa, na Myahudi.

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Danieli 6:7, 10-11 na ueleze sababu ya kutolewa kwa sheria ile.

Eleza kwamba sehemu hii ya hadithi ya Danieli ilitokea miaka mingi baadaye. Alikuwa yungali kijana alipopelekwa Babeli, na alipofanywa mtawala. Hata hivyo, inafikiwa kwamba Danieli alikuwa na umri wa miaka themanini wakati sheria hii ilipopitishwa.

Uliza: Je! sheria hii ingekuwa na nguvu kwa muda wa siku ngapi? (siku thelathini)

Sema: Sheria haingebadilishwa baada ya kupitishwa. Huu ndio uliokuwa mtindo wa Wamede na Waajemi. (Esta. 1:19 inaeleza juu ya jambo hili.)

Uliza: Je! Danieli alionyesha je ujasiri wake? (Alienda nyumbani kwake na akaendelea kuomba mara tatu kwa siku.)

Uliza: Je! Unafikiri ungeweza kumshukuru Mungu iwapo ungekuwa mahali pa Danieli? (Wape muda wa kujibu.)

Uliza: Je! Ni nini kingefanyika iwapo ungeomba kila wakati ukimtaka Mungu akupe hekima ya kuibadili shida yako? (Mungu angekupa ujasiri wa kusimama imara kwa ajili yake jinsi alivyomsaidia Danieli.)

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Danieli 6:16-23. Eleza kwamba Tundu la Simba lilikuwa shimo kubwa lenye sehemu ndogo iliyo wazi kama mdomo wa chupa. Sehemu kama hizi zilitumiwa kwa kuhifadhi maji, au kutumiwa kama jela.

Uliza: Je! mfalme alifikiria je juu ya hali hii ya Danieli? (Alitamani kumwokoia lakini hakuweza, ila alimhimiza tu kwamba atasaidiwa.)

Uliza: Je! Mungu alimsaidia je au alimponyaje Danieli kutoka kwa simba? (Alituma malaika wake kuyafumba makanwa ya simba.)

Uliza: Je! ni nini kilichotokea kufuatana na imani ya Danieli kwa Mungu? (Mungu alimwokoia na akawafanya waliomshitaki wateswe. Sheria mpya ilipitishwa iliyosema kwamba kila mtu aabudu na kumtumikia Mungu wa Danieli.)

Sema: Danieli alifanya kazi yake vizuri na alipewa cheo cha heshima. Alitumika wakati wa wafalme watatu na alikuwa mwaminifu kwao. Hali, hakuifikiria kwanza huduma ya mfalme kuliko ya Mungu. Hakuacha kuhatarisha maisha yake ili kusimama imara kwa yale aliyoamini. Hata ingawa alikuwa akiokolewa kila wakati, yeye alikuwa tayari kufa.

KAZI YA KUFANYA

Soma Maandiko uliyopewa na ujibu maswali hayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa.

1. Danieli 6:7. Je! ni sheria ipi ambayo mfalme alitia sahihi? "...mtu ye yote atakayeomba dua kwa Mungu awaye yote, au kwa mtu awaye yote, katika muda wa siku

thelathini, ila kwako, Ee mfalme,
atatupwa katika tundu la simba.”

2. Danieli 6:10. Je! Danieli alifanyaje aliposikia habari za sheria hii? Danieli aliingia nyumbani mwake, akapiga magoti mara tatu kila siku na kuomba.

3. Danieli 6:14. Je! Mfalme alijisikiaje alipoambiwa kwamba Danieli alikuwa amevunja sheria hii? Alisikitika sana na akajaribu kutafuta njia ya kuweza kumwoko Danieli.

4. Danieli 6:18. Je! Mfalme alifanyaje kuonyesha kwamba alihuzunika sana wakati Danieli alipotupwa kwenye tundu la simba?

Alienda nyumbani kwake, akakesha usiku kucha, akafunga, wala hakupata usingizi.

5. Danieli 6:19-20. Je! mfalme alifanya nini kulipokuwa asubuhi na mapema?

Alienda kwa haraka mpaka penye lile tundu la simba na akamlilia Danieli akisema, “Ee Danieli mtumishi wa Mungu aliye hai, Je! Mungu wako unaye-mtumikia daima, ameweza kukuponya na Simba hawa?”

6. Danieli 6:23b. Je! Kwa nini Danieli hakudhuriwa?

Ndipo Danieli alipotolewa katika lile tundu, wala dhara lo lote halikuonekana mwilini mwake, kwa sababu alikuwa anamtumainia Mungu wake.

Andika sentensi zifuatazo kulingana na vile zilivyofanyika. Andika namba 1

kuanzia lile jambo lililofanyika kwanza na uendelee vivyo hivyo hadi mwisho. Umejaziwa nafasi ya jibu la kwanza.

2 Danieli na rafiki zake watatu walikataa kula chakula cha mfalme.

5 Danieli alitupwa kwenye tundu la simba.

1 Danieli alipelekwa Babeli kama mfungwa.

4 Watawala wa mfalme walimpata Danieli akiomba.

3 Danieli alikuwa mmojawapo wa watawala wa mfalme Dario.

6 Mfalme alipitisha sheria kwamba kila mtu atapaswa kumwabudu Mungu wa Danieli.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

“Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Bwana ngome ya uzima wangu, nimhofu nani?” (Zaburi 27:1).

Waambie wanafunzi waseme baadhi ya hofu au woga walionao. Wahimize wamwombe Mungu wakitumia kifungu walichopewa katika kitabu chao cha wanafunzi.

Andika maneno ya kifungu hiki kwenye vijikaratasi jinsi ifuatavyo:

BWANA NI NURU YANGU
NA WOKOVU WANGU:
NIMWOGOPE NANI?
BWANA NI NGOME
YA UZIMA WANGU,
NIMHOFU NANI?

Waambie wanafunzi sita wachague kijikaratasi kimoja halafu wasimame na kujipanga jinsi maneno ya kifungu hicho yanavyofuatana.

WAKATI WA MWISHO

Uliza: Je! kunaye ye yote ambaye ana ushuhuda wa kutoa jinsi Mungu alivyombariki au alivyomlinda? (Wape wanafunzi hao nafasi ya kuweza kuelezea yale ambayo Mungu amewafanyia.)

Sema: Taja baadhi ya mambo ambayo yanaweza kukujaribu ili usiwe mwaminifu kwa Mungu.

(1) Kutokuwa na marafiki fulani, kutoenda katika sherehe au kuwa katika kundi fulani la watu.

(2) Kudhihakiwa kwa kuwa u Mkristo.

(3) Kuhimizwa kutumia madawa ya kulevyu au kunywa pombe.

(4) Kujisikia tofauti iwapo hushiriki katika mambo ya usherati.

Uliza: Je! uko tayari kuwa kama Danieli? Alimwamini Mungu ambaye aliweza kumwokoa wakati wa shida.

Sema: Mungu anawataka watu ambao watasimama imara kwa niaba yake wakiwa nyumbani, shuleni na katika taifa letu jinsi Danieli alivyofanya.

MAMBO YA MWISHO

Waambie wanafunzi hao wa-mwombe Mungu kimoyomoyo ili aweze kuwasaidia katika kumwamini yeye wakati wawapo na shida au matatizo.